

NA TUMWONE MUNGU



Ketini. Samahani kwa kufanya hivyo, Ndugu Borders, bali kulikuwako na kisa cha dharura papo hapo nje, alikuwa akifa kwa kansa, na ilinibidi tu kumfikia. Ninii tu... Najua mtanisamehe hilo. Kwa hiyo, ni sawa. Nilichukia kuchelewa. Nilikuwa nikingojea kwa muda kidogo tu, na kukutana na baadhi ya marafiki, ndipo nikafikia kisa hiki ambacho ndio kwanza kiletwe, mahututi sana, sana, kwa hiyo ilinibidi kukiendea upesi sana.

² Sijui tu jinsi ya kuanza, alasiri ya leo. Nilikuwa nikiwazia nikiwa njiani kuja huku, “Nitaliambia nini ku—kusanyiko la watu kama hawa?” Huu umekuwa ni mkutano muhimu sana kwangu. Na sisemi hilo kwa sababu tu niko mbele zenu. Ninasema hilo kwa sababu linatoka moyoni mwangu. Nami ninataka kila mmoja wa hawa wahudumu kujua ya kwamba ninauchukua huu kama mmoja wa mikutano yangu mikuu sana niliyowahi kuwa nayo. Hiyo ni kweli. Kwa sababu ya ushirikiano wenu mwema ndio uzuri wake. Nimeona nyakati ambapo kulikuwa na... Nimekuwa na idadi kubwa zaidi katika kusanyiko, mahudhuri makubwa zaidi, bali sijapata kuona mkutano niliopata kuwa nao maishani mwangu wenye ushirika mtamu sana kuliko ule nimekuwa nao miongoni mwenu ndugu. Mungu awabariki. Ninatumaini ya kwamba makanisa yenu yatakua na kupanuka mpaka hapatakuwako na mwisho wake. Ninaomba ya kwamba Mungu atawaweka katika huduma mpaka atakapokuja. Hili ndilo ombi langu aminifu kwa ajili yenu. Na mimi—mimi hata nimekuwa na wakati nimekuwa na wahudumu wengi zaidi wakishirikiana, kama vile wakati mwingine huko Afrika, India, namna hiyo, wakati tungekuwa na mia kadhaa kwenye halmashauri. Lakini kamwe si wakati kama huu, inaonekana, nyuma yangu, moyo mmoja na nia moja. Hiyo ni ajabu kweli. Ninathamini jambo hili, ndugu. Na bila shaka mimi, jambo lolote ningaliweza kuwafanyia, kumbukeni tu mimi ni ndugu yenu. Usiku hauwi na giza kupita kiasi, mvua haitanyesha kwa nguvu kupita kiasi, mnaona, nitafanya lolote niwezalo kuwasaidia kuiendeleza Injili hii kuu ama kuwafanyia jambo fulani. Mungu daima awe pamoja nanyi!

³ Ninataka pia kusema, kwa maskini ndugu yangu hapa, Roy Borders, nimemfahamu Ndugu Borders kwa muda mfupi tu. Sikuzote nimetamani kumpata mtu ambaye angeniandalia mikutano. Ndugu Roy alionekana kupashika mahali hapo. Yeye si mhudumu. Yeye ni mfanyabiashara. Nimemwacha aandae mikutano miwili au mitatu, kuona tu yale angeweza kufanya, na haya ndiyo matokeo yake: nia moja. Na kwa kawaida kama mhudumu akija kuandaa mikutano kwa ajili yako, vema, daima

kuna mhudumu aliye na jambo moja ama lingine, naye ana fundisho ama—ama kitu kingine ambacho—ambacho anataka kuwasilisha. Naye anaingia miongoni mwa wahudumu na kuwasilisha fundisho lake, ndipo—ndipo uko taabuni. Mnaona? Kwa hiyo, ni bora kwa mtu asiye mhudumu.

⁴ Jambo lingine, nikiingia, mtu fulani aliniuliza, kasema, “Ndugu Branham, kwani wewe ni Jesus Only, wewe ni mfuasi wa Jesus Only?”

⁵ Nikasema, “La hasha.”

⁶ Kisha kasema, “Mtu fulani alisema wewe huamini katika kunena kwa lugha.”

⁷ Nikasema, “Hawanijui vizuri sana, hivyo tu. Hakika, ninaamini.”

⁸ Sasa, naye Ndugu Borders hakika ni Mkristo muungwana, amefanya kazi nzuri sana. Nami hakika ninamshukuru Ndugu Borders kwa kunialika. Yeye amekuwa na huzuni nyingi, matatizo mengi, bali ame—amefanya kazi nzuri. Mungu ambariki Ndugu Borders, ndilo ombi langu aminifu.

⁹ Ndugu Wagner, nafikiri kwa njia fulani yeye ni mwenyekiti, naamini. Ndiye nimekuwa nikikutana naye sikuzote, wa kamati. Kazi nzuri sana, kama tu vile alivyofanya wakati ule mwingine, vizuri. Alinalika huko nyumbani kuwa pamoja naye, niketi nyumbani mwake. Hakika nilitaka kufanya hivyo sana, karibu ningeweza kulihisi. Ilibidi kumkatalia kwa sababu nilidhani labda, pamoja na ushirika huu mzuri sana, ningetaka kuja kwa kila moja ya nyumba zenu, mnaona, napenda kumwona kila mmoja wenu. Nami ni—niliziheshimu hisia zenu, nami nina hakika Ndugu Wagner alielewa jinsi ilivyokuwa hasa, mnaona. Kwamba mimi . . . kama nikienda kwa Ndugu Wagner, ningependa kwenda kwa kila mmoja wenu namna hiyo. Kama nisipoweza kufanya hivyo, Ndugu Wagner, siku moja kwenye ng'ambo ya pili, kwenye ng'ambo ya pili tu, ninataka miaka elfu moja, kila mmoja, pamoja na kila mmoja wenu. Kwa hiyo tutakuwa tu na wakati mzuri sana Kule!

¹⁰ Ndugu Toy, yeye hakika, yeye ni ninii tu . . . Sioni jinsi anavyofanya mambo mengi hivi kwa wakati mmoja, lakini hakika anaweza kukamilisha mengi sana. Nilimwona hivi majuzi kwenye kiamshakinywa cha Wafanyabiashara, jinsi alivyokuwa akichukua mahali pa mhubiri, shemasi, bawabu, na chochote kile kilichotokea, naye alikuwa akijaribu kufanya hayo yote. Yeye anampenda Bwana. Nilikuwa na majaliwa ya kukutana na mke wake, na kumwona binti yake mpendwa na mumewe wakiimba. Bila shaka ilikuwa inatia moyo. Nilimwambia tu, dakika chache zilizopita, “Hawana haja ya kuwa nyumbani, wakifanya kazi ya kawaida. Wanapaswa kuwa nje kwenye huduma ya kiinjilisti mahali fulani, wakiwa na karama kuu kama hizo.”

¹¹ Mnaona, kila mmoja anayo, natumaini simwachi mtu yeyote nje. Mama anayecheza piano, hao waimbaji, hizo kwaya, na wote ambao wamekuwako, hakika ninawathamini kwa moyo wangu wote.

¹² Nao hawa wavulana hapa, Gene na Leo, wanataka kuelezea hisia zao kwenu, pia, kwa ajili ya kununua kanda na vitabu, na sehemu inayowapasa kushughulikia. Ndio kwanza nikutane nao mlangoni, dakika chache zilizopita, nami nikawaambia ningeelezea hisia zao kwenu enyi watu. Bila shaka wanathamini kila kitu ambacho mmefanya kwa kuwasaidia pamoja na huduma kuu ya Mungu.

¹³ Na sasa hili linatoka kwangu mwenyewe, mwanangu, mke wangu, na binti mkwe wangu, na wote. Wengi, mtu fulani amekuwa akisema, “Dada Branham ni nani?” Huyu ndiye msichana mwenye soni kuliko wote niliyepata kumwona maishani mwangu mwote. Loo, jamani!

¹⁴ Ndugu Art Wilson, nina hakika ninyi nyote mnamfahamu. Ninaamini ilikuwa ni ndugu... La, ilikuwa ni Ndugu Jewel Rose, usiku mmoja, aliyesema, “Tutamwalika Dada Branham aje hapa juu jukwaani,” naye karibu ashikwe na mshtuko wa moyo. Alininii tu... Yeye ni mwenye soni kwelikweli.

¹⁵ Kipenzi, endapo hutazimia, waweza kusimama tu kwa dakika moja, ili kwamba mtu fulani aweze kuona ni msichana mzuri jinsi gani niliyemwoa. Vema. [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Binti mkwe wangu, mke wa Billy, Loyce, naomba usimame, Dada, kwa dakika moja tu. Huyu ni mke wa Billy, [Kusanyiko linashangilia.] na binti mkwe wangu.

¹⁶ Wengi wenu mmesikia habari za Joseph. Sivyoy? Waafrika hivi majuzi walimtumia koti dogo lenye rangi kadhaa. Nilimwona miaka sita kabla hajaja, wakati daktari aliposema kamwe hatutampata mtoto mwingine, tusingeweza kumpata. Ilibidi watoto wetu wazaliwe kwa upasuaji. Mama yangu, watu wa mke wangu wako hivyo, wao, watoto wao wote huzaliwa kwa upasuaji. Naye Bwana aliniambia ya kwamba nitampata mtoto huyu mchanga, wakati daktari alisema isingewezekana, alisema kamwe isingewezekana. Nikasema, “Itakuwa, kwa vyovyote vile.” Nasi tukangojea kwa muda wa miaka minne, baada ya ono kutokea kwamba ningempata mvulana, nami ninapaswa “kumwita jina lake ‘Joseph.’”

¹⁷ Ndipo, baada ya hapo, kulikuwako na msichana mwingine aliyezaliwa. Kila mtu akanicheka, na kusema, “Ulimaanisha ‘Josephine.’”

¹⁸ Nikasema, “La. Nilimaanisha ‘Joseph,’ akiwa ni mvulana.” Labda atapachukua mahali pangu nikiisha kuondoka, Yesu akikawia. Basi miaka minne zaidi; daktari alikuwa na hakika kamwe kusingekuwako na mwingine; miaka minne zaidi, Joseph akawasili.

¹⁹ Nashangaa, mami, endapo ungeweza kumwinua juu kwa dakika moja. Ninataka waone vile... Mvulana huyu tayari yuna roho ya unabii juu yake. Naye... Simama kidogo tu, Joseph. Huyo *hapo*. Vema. [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Yeye ni kama mama yake, mwenye soni.

²⁰ Nitawaambia kilichotukia. Tulikuwa mbali, ana umri wa miaka minne sasa, lakini alipokwa na mitatu, tulikuwa mbali, naye akasema, “Baba?”

Nami nikasema, “Naam, kipenzi?”

²¹ Akasema, “David...” Huyo ni yule mvulana aliyekuwa kiwete, naye akaponywa, mwana wa Bw. Wood anayeishi jirani yetu. Kasema, “Nilikuwa... nilimwona amepata ajali akiendesha pikipiki.” Yeye hata hana pikipiki. “Nayo ikaujeruhi mguu wake, akararua nguo zake mkono wa kuume.”

Nikasema, “Hiyo ilikuwa ni wapi, kipenzi?”

²² Kasema, “Kwenye ile njia ya miguu kutoka mahali tunapoishi.” Ndipo siku tatu baadaye, mvulana mmoja alipita kule kutoka Kentucky, akiendesha pikipiki, naye David akashuka kwenye ile njia ya miguu na kujeruhi upande wake wa kuume na kuzirarua nguo zake, jinsi tu Joseph alivyoliona.

²³ Nilipomweka wakfu kwa Bwana, ile asubuhi, kulikuwako na watoto wengi wachanga waliosimama, nao walikuwa na mama pamoja nao madhabahuni, nilipomchukua Joseph mikononi mwangu, pasipo kuwazia nililokuwa nikisema, nilisema, “Joseph, mwanangu, wewe ni nabii.” Hilo ndilo ombi langu, kwa vyovyote vile, nami ninaamini itatimia, kwamba, Mungu atachuka kila kitu alichopata kunipa mimi, na kukijumlisha maradufu mara maradufu, na kukiweka juu ya mvulana huyo, ndipo nitakapoondoka yeye atapachukua mahali pangu.

²⁴ Billy amekuwa sahibu wangu. Nimemlea; mama yake alikufa wakati akiwa na umri wa miezi kumi na minane; nami nimekuwa baba na mama, wote wawili, kwake. Lakini inaonekana kana kwamba yeye hana wito kuwa mhubiri. Yeye ana haya, ni wa kujiweka nyuma, na kadhalika, zaidi sana kama mama yake, mwenye haya. Lakini amekuwa msaada mkubwa kwangu mkutanoni, maana nimemtumainia, kumpeleka huko nje na kumpa kazi yenye wajibu mkuu. Mnaona, hiyo kazi ya kadi ya maombi ni kazi yenye wajibu mkuu. Mtu fulani akiipata hiyo na kusema... Mtu mmoja wakati mmoja alisema, “Nitakupa dola mia tano kama utamweka mke wangu jukwaani.” Vipi kama hilo lingetendeka? Basi ingekuwa kwa Roho Mtakatifu? Billy anajua vema vya kutosha kutojaribu hilo. Angejua ningejua mara afikapo jukwaani, kwa hiyo, Bwana angelifichua. Hiyo ndiyo sababu kamwe a—asingefanya hivyo, kwa hiyo basi sote tunakushukuru.

25 Halafu kwa msimamizi, yule muungwana anayetusaia pale langoni, nami nafikiri kwa namna fulani ndiye msimamizi hapa, ama kitu kama hicho, ama mlinzi langoni. Na kwa watu wote walioturuhusu kuchukua ukumbi huu mzuri, kamwe siwezi kusema “asante” vya kutosha. Bila shaka nathamini hilo, na yote hayo kwa kila njia, na kila kitu kinachofanywa.

26 Sasa waliniambia, Ndugu Borders, muda mfupi uliopita, ya kwamba walichukua sadaka ya upendo kwa ajili yangu. Ninathamini hilo, na kwa moyo wangu wote. Nitazitumia, nijuavyo mimi, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Sasa, si yale tunayoweka hapa ndiyo muhimu, ni yale tunayotuma nje. Nami nina hakika Mungu ataweka hayo kwenye akiba yenu kwenye Ufalme ujao.

27 Sasa, sina kipindi cha redio. Sina chochote cha kuuza. Lakini kama kamwe ukihitaji moja ya hizi lesi ama kitu cha kuombewa, niandikie kwenye Jeffersonville, Indiana, Sanduku la Posta 325. Kitahudumiwa, kibinafsi, na kurudishwa kwako moja kwa moja. Nami ninaamini katika huduma hiyo. Halafu kama kamwe ukihitaji kunipigia simu, BUTler 2-1519 itanipata huko Jeffersonville, Indiana. [Nambari ya simu imebadilishwa—Mh.] Kwa hiyo, ama endapo huwezi kuikumbuka hiyo, niulizie tu huko Jeffersonville, watanipigia simu. Sasa, sifanyi hivyo nipate anwani yenu, kwa sababu nina wakati mgumu kumpata mtu wa kunijibia barua, na kadhalika. Na sasa sina ninii sana . . . Ni sawa, ninaamini katika mipango hii. Kila kitu kitakachomsaidia Mungu, na kiwe.

28 Lakini, mwajua, ninajisikia namna hii, ya kwamba mfuasi wa kanisa, jukumu lao la kwanza ni, pamoja na zaka zao na matoleo, ni kulisaidia kanisa lao. Iwapo nyinyi ni wafuasi wa moja ya makanisa haya mazuri yaliyowakilishwa hapa, wewe lisaidie kanisa lako, hilo ndilo jukumu lako la kwanza kwa Mungu, “Leteni zaka na matoleo yenu ghalani.” Nalo ghala, hakika mnajua hilo ni nini, ni mahali unapopata chakula chako, basi *hapo* ndipo unapopata Chakula chako cha kiroho. Na jukumu lako ni kwa kanisa lako wala sio kwa mwinjilisti kama mimi.

29 Inachukuliwa mahali fulani mikutanoni wakati tunapokuwa na miamsho kama huu, ambapo mna kidogo kilichowekwa kando kuisaidia, hicho kinanishughulikia. Nami nawashukuru sana. Na kila wakati, vitambaa vya maombi ama chochote kama hicho, ni bure kabisa. Hakuna kitu ndani yake hata kidogo, hatuninii . . .

30 Navyo vitabu vyetu, na kadhalika, tunapoviuza, hivyo ni . . . Inatubidi kuvinunua, asilimia arobaini chini ya kile tunachopata kwavyo, na kisha sisi . . . hiyo ni, kupitia pale, unapata hasara nyingi kwavyo, kisha unalipia malipo ya kuvituma licha ya hayo, halafu inakubidi kuvisafirisha hapa na halafu uviuze.

Mbona, usingeweza, usingeweza kupata faida kwake hata ufanyeje, mnaona. Lakini tunafanya hivyo kusudi tuwalettee huu Ujumbe, kujaribu kuwafanya msaidike, ninyi wenyewe; kisha muwaambie mtu mwingine, na kuwapelekea. Hiyo ndiyo kazi ya vitu hivi, sivyo? Ukomunisti hutoa vitabu vyao na maandishi yao, bure, kwa sababu hao ni mfumo mkuu wa utawala. Mimi ni mtu mmoja tu. Laiti ningaliweza, ningalikuwa na pesa nipate kusema “vitabu vyote na kila kitu, bure,” ningefanya hivyo. Lakini siwezi kufanya hivyo, sina budi kupata kitu cha kurudi na kuchapisha vingine zaidi, ama—ama kununua vingine zaidi.

³¹ Bwana awabariki. Nanyi mtaniombea, sivyo? Ndipo wakati nikiwa kwenye nchi za ng'ambo, na katika sehemu hizo zenye giza ambako wachawi wemesimama kila mahali, wanakupa changamoto kwa kila kitu unachosema, nyakati ni ngumu, upepo wenye joto wa mateso unavuma, je, ninaweza kuwaweka kwenye orodha, ama ninyi mniweke kwenye orodha yenu, nami ninaweza kukumbuka wakati inaponibidi kukabiliana na changamoto hiyo ya wachawi na ibilisi, na vitu huko nje hudumani, ninaweza kusema, “San Jose inaniombea”? Mtaniombea, mtafanya hivyo? Inua mkono wako kama utaniombea, useme, “Nitakuwa nikikuombea.” Asante. Asanteni, ndugu zangu. Asanteni. Nimekuja miongoni mwenu, kuwa ndugu yenu, na kuleta... kusaidia kuleta amani pamoja na Kristo, kila kitu kilicho kizuri kwenu. Ninyi niombeeni. Iwapo nimemwacha mtu yeyote, samahani, simaanishi kufanya hivyo. Lakini “asante” kubwa ya moyoni, na baraka za Mungu kwa kila mmoja wenu.

³² Inatupasa kuondoka kwenda nyumbani sasa, sasa hivi. Nina yapata mkutano wa siku tatu katika maskini kanisa langu, kuwafundisha ubatizo wa Roho Mtakatifu, kunena kwa lugha, ishara na maajabu kuwafuata waaminio, na kadhalika; kwa watu walio huko, mle ndani.

³³ Ninaamini katika karama zote za kiroho. Ninaiamini Biblia yote. Mimi ni Mpentekoste kutoka juu ya kichwa changu hata chini ya miguu yangu, ndani, nje, kote kote, kila mahali. Mimi ni Mpentekoste! Naam, bwana! Wao wanasema, “Wewe ni ‘Mbaptisti,’ ulisema.” Mimi ni Mbaptisti Mpentekoste. Mimi ni Mbaptisti aliyecipata Baraka za Kipentekoste. Kwa hiyo mimi... Ninampenda Bwana Yesu.

³⁴ Nami nilikuwa nikihubiri... Nikakutana na baadhi ya marafiki kutoka Arkansas, huko nje, nasi tulikuwa tukizungumza juu ya Arkansas. Na huko Little Rock, usiku mmoja wakati... Kulikuwako na maskini ndugu Mnazarayo aliyekuwa akitembea kwa magongo, naye alikuwa ameua penseli mtaani, kwa miaka kadhaa. Naye huyu hapa nje mtaani, kesho yake, akiwa na maskini magongo haya, akitembea huku na huku mtaani, akimtukuza Mungu tu. Usiku huo alikuwa... Ukumbi wa Kumbukumbu wa Robinson, ninyi watu mnaotoka karibu na Little Rock mnajua mahali ulipo. Ndi—ndipo akainua

mkono wake, na kusema, “Hebu kidogo, Ndugu Branham, ninataka kukuuliza jambo fulani.”

Nikasema, “Naam, bwana, ni lipi?”

³⁵ Akasema, “Unajua, nilipokusikia ukihubiri, nilikuwa na uhakika ulikuwa ni Mnazarayo.” Maana, hivyo ndivyo alivyokuwa. Akasema, “Nilikuwa na hakika wewe ni Mnazarayo, maana unahubiri kama tu Mnazarayo.” Kisha kasema, “Ndipo nikasikia ukisema ulikuwa mfuasi, wakati huo, wa kanisa la Baptisti.” Halafu kasema, “Kusanyiko lako lote, karibu lote, ni la Kipentekoste.” Kasema, “Sielewi hilo.”

³⁶ Nikasema, “Vema, hilo ni rahisi. Mimi ni Mbaptisti Mnazarayo wa Kipentekoste.” Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo. Jambo lote ni hili: sisi ni mmoja, katika Kristo Yesu, tumefungwa kwa vifungo vya upendo Wake.

³⁷ Na tuombe sasa kabla hatujalifungua Neno, hatutaki kuwaweka muda mrefu sana sasa hata mkachelewe kwa ibada yenu ya kanisa usiku wa leo. Lakini hebu tumwombe Mungu sasa aingie na kutubariki kwa wingi, sana. Ni wangapi walio na haja sasa, inueni mikono yenu na kusema, “Bwana Mungu, nikumbuke tu, mimi—mimi ni mhitaji leo hii”? Mungu awe nanyi.

³⁸ Baba wa Mbinguni, huku tukiukaribia Uwepo Wako Mtakatifu tena, tuna-. . . la, na, tunajisikia tu kuvivua viatu vyetu, lakini tunaitoa mioyo yetu na kuiweka tu mbele Zako, Baba. Tunakushukuru kwa yote ambayo umefanya katika uamsho huu mkubwa. Tunatambua, Bwana, ya kwamba ukuu haumaanishi idadi. Ukuu ni Uwepo Wako. Kwa kuwa, iliandikwa kuhusu Masihi ajaye, ya kwamba, “mahali pote palipoinuka patashushwa, na mahali paliposhushwa patainuliwa; matawi yatapiga makofi yao, nayo milima itarukaruka kama ndama wadogo.” Ndipo mtu angewazia katika mawazo yao ya kiakili, juu ya ule wakati mkuu ujao, kwamba magari ya moto yangeshuka kutoka Mbinguni, yakimleta Masihi. Lakini ilitukiaje? Kwa maskini mhubiri aliyeonekana mkali, akitoka katika nyika ya Uyahudi, hata hajavalia kama mhudumu; amevikwa kipande cha ngozi, kama ngu—nguo; amejaa nywele, na ndevu zake zimejaa usoni mwake; akihubiri, sio kanisani, bali ufukoni mwa Yordani, akipaza sauti, “Tubuni, kwa kuwa Ufalme wa Mungu umekaribia!” Chini kwenye ufuko uliojaa matope, zilikuja nyayo za Seremala wa Galilaya, aliyeingia majini, naye Mungu akazitambua na kuziheshimu hata akafungua Mbingu nao wakamwona Roho Mtakatifu akishuka kama hua juu Yake. Hilo lilikuwa ni jambo kuu. Kile mwanadamu anachoita “kikuu,” wakati mwingine ni upumbavu machoni Pako, Bwana. Lakini kile mwanadamu anachoita “kipumbavu,” ni kikuu machoni Pako.

³⁹ Sasa tuna furaha sana ya kwamba jambo kuu limetukia katika San Jose. Hapa wameketi wahudumu wanaoketi hapa, baadhi yao ni wa Assemblies of God, baadhi yao ni wa Church of God, Independent, na United Pentecostals, na aina zote mbalimbali. Nami hapa nimesimama kati yao, bila kuwa mfuasi wa dhehebu lolote, bali ninajaribu kusimama katika pengo, nikizungumza kwa niaba ya wote. Nasi ni mmoja, ndani Yako; moyo mmoja, nia moja, mahali pamoja. Ni wakati wa jinsi gani kwa Roho Mtakatifu kufanya upya kitu fulani! Lijalie, Bwana. Kuwa pamoja nasi, Bwana. Bariki kila dhehebu lililowakilishwa hapa. Tujalie, Baba. Wahudumu hawa wote wazuri, jalia makanisa yao yakue na kufanikiwa, Bwana. Wagonjwa na waponywe, vipofu waone, viziwi wasikie, wenye dhambi waokolewe na kujazwa na Roho Mtakatifu. Jalia pawe na uamsho utakaotokea kote kwenye nchi hii hapa, ambao utaitikisa Pwani nzima ya Magharibi. Lijalie, Bwana. Jalia bidii kubwa sana itokee miongoni mwa ndugu zangu, hata kamwe hawawezi kupumzika; mmoja atamtia moto huyo mwingine, na kila kanisa litaendelea mbele kama umoja mkuu, wakishirikiana wao kwa wao, wakimega mkate nyumba kwa nyumba, kwa umoja wa moyo. Tujalie, Bwana. Utume huo uamsho tunaoungojea.

⁴⁰ Libariki kusanyiko, wanapongojea alasiri ya leo uponyaji wao, na wengi kwa ajili ya wokovu wao. Pia unisaidie mimi, Ee Mungu, ninaposoma kutoka kwenye Maneno Yako matakatifu. Jalia Roho Mtakatifu achukue kilicho Chako, Bwana, na kukileta mionyoni mwetu. Kisha anitumie mimi, Bwana, kutoa sehemu inayoridhisha ya Neno Lako kwa kila moyo wenye njaa. Nisikie, naomba, Baba, katika Jina la Yesu naomba hayo. Amina.

⁴¹ Mtu fulani ndio kwanza anipe muhtasari mdogo, na kusema, “Ndugu Baxter, kutoka Canada, anatuma upendo wake na salamu kwako, naye yuko hapa California sasa, akifanya mkutano huko Concord.” Mungu ambariki Ndugu yetu Baxter. George Patterson, uko hapa? George Patterson, uko humu mkutanoni? Iwapo uko, peleka upendo wangu. . . Mungu akubariki Ndugu Patterson; peleka upendo wangu kwa Ndugu Baxter, mtu mzuri. Na endapo yeyote wenu yuko karibu na huko, kama ukitaka kusikia mahubiri yakihubiriwa na mtu anayejua jinsi ya kuhubiri, nenda kamsikilize, endapo uko karibu na kule; bila shaka ni mhubiri mzuri sana. Tulikuwa pamoja kwa muda wa miaka mingi, mingi sana. Upendo wangu kwa Ndugu Baxter haujafifia; hautafifia kamwe. Yuna kanisa kubwa huko Canada. Asingeweza kuwa pamoja nami tena, kwa sababu ya mahitaji ya kanisa lake.

⁴² Ninajua hilo ni nini. Hata Maskani yangu leo hii, ambayo wakfu wangu. . . Sasa, watu wanaotuma michango kwa wakfu huu, wanayo namba ya serikali inayokurudia, kukupa msamaha wa kodi kwa zote unazotuma kwenye wakfu huu. Ni—ni wakfu

usio wa kupata faida, unaoitwa Branham Tabernacle. Nami ninajua, hapo, hao wadhamini wananisukuma sana, “Hebu tujenge maskani kubwa, wewe ubaki hapa uache watu waje kwako.” Hilo linasikika sawa, bali hilo si mapenzi ya Mungu kwangu. Kuna watu ambao hawana pesa za kutosha kuja kwangu, inanibidi kwenda kwao. Mnaona? Kwa hiyo ni—ninajua jinsi ilivyo kuwekewa presha.

⁴³ Naye Ndugu Baxter aliwekewa hiyo, kwa hiyo ilimlazimu kuondoka kwenye uamsho na kwenda kwenye kanisa lake. Bwana ambariki Ndugu yetu Baxter. Mpelekee upendo na salamu zangu, binafsi, kwa niaba yangu, tafadhali, ndugu.

⁴⁴ Sasa hebu tuyafungue Maandiko, kwa dakika zingine kama ishirini, kwenye baadhi ya Neno, ambalo, kamwe halitashindwa. Na watu wote walio hapa, wagonjwa, wanaohitaji chochote, jiachilieni tu mwingie moja kwa moja kwenye Neno. Nilikuwa nikitaka kuhubiri alasiri ya leo juu ya *Kama Tai Ataharikishavyo Kiota Chake*, lakini, ninakuta kwamba, hawa wavulana waliuleta hapa na kuuza miongoni mwa watu, katika umbo la kitabu. Halafu, kwa kuwa kidogo nina mkwaruzo kooni mwangu, nilichukua somo lingine. Nami nafikiri sasa nimetaja kila kitu ambacho nilipaswa kutaja. Vema. Hebu tufungue katika Yohana Mt., mlango wa 14, kwa somo letu la Maandiko. Basi sikilizeni kwa makini tunaposoma vifungu vya kwanza vinane vya Yohana 14.

Msifadhaike mioyoni mwenu: mnamwamini Mungu, niaminini na mimi.

Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi: kama sivyo, ningaliwaambia. Maana naenda kuwaandalia mahali.

Basi nikienda kuwaandalia mahali, nitakuja tena, niwakaribishe kwangu; ili nilipo nanyi mwepo.

... niendako mnakujua, na mwaijua njia.

Tomaso akamwambia, Bwana, sisi hatujui ni wapi uendako; basi twaijua njia?

Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, kweli, na uzima: mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.

Kama mngalinijua mimi, mngalimjua na Baba yangu: tangu sasa mnanijua, tena mmeniona mimi.

Filipo akamwambia, Bwana, utuonyeshe Baba, yatutosha. (Kwa maneno mengine, “yaturidhisha.”)

⁴⁵ Sasa hilo ndilo ninalotaka kuzungumzia, alasiri ya leo. Kimekuwa ni kilio cha moyo wa binadamu, kwa ajili ya... tangu tumekuwa binadamu, tungetaka kumwona Mungu. Nami ninataka kuchukua yapata njia nne, alasiri ya leo, kuwaonyesha Mungu. Kwanza ninataka kumchukua Mungu katika ulimwengu Wake, Mungu katika Neno Lake, Mungu

katika Mwanawe, Mungu katika watu Wake. Nasi tungeweza kulichukua njia zingine nyingi. Lakini ningetaka kuzungumza kutoka kwenye masomo hayo manne, njia nne mbalimbali ambazo tutaziangalia, kuona kama tungeweza kumwona Mungu. Sasa, hakuna mtu hapa ila yule ambaye angependa kumwona Yeye. Hivi msingetaka kumwona Mungu? Ningetaka kumwona. Kwa hiyo ikiwa Yeye ni Mungu, ambaye tunajua kwamba ndivyo alivyo, basi kwa nini tusiweze kumwona?

⁴⁶ Ayubu wakati mmoja alisema hivyo, kile Kitabu cha kale kuliko vyote katika Biblia, kilisema kitu kama hiki, “Laiti ningalijua mahali anapoishi, ningeenda niubishe mlango Wake. Nami ningetaka kuzungumza Naye.” Naye akapata kuzungumza na Mungu. Mungu alimwambia ajifunge mshipi kama mwanaume, kwa kuwa alikuwa anaenda kuzungumza naye. Naye akashuka kwenye upepo wa kisulisuli, kisha akazungumza na Ayubu.

⁴⁷ Inanikumbusha juu ya ninii...kule karibu na kwetu. Tunaishi kwenye Mto Ohio. Basi kulikuwako na mvulana mdogo aliyehudhuria Shule fulani ya Jumapili, Shule ya Jumapili ya Baptisti, nchini mwetu, naye alisisimkwa sana. Siku moja wakati alipomuuliza mama yake, “Iwapo Mtu huyu mkubwa anayeitwa Mungu, ambaye tunaenda kanisani kumwabudu, iwapo Yeye ni Mtu mkuu hivi, sijui kama mngenionyesha? Ningetaka kumwona.”

⁴⁸ “Loo,” mama akamwambia mtoto wake mdogo, akasema, “vema, mwanangu, inakupasa kumwuliza mwalimu wako wa Shule ya Jumapili, mama hawezi kukupa jibu hilo.”

⁴⁹ Kwa hiyo kwenye Shule ya Jumapili alizungumza na mwalimu wake, naye akasema, “Sina uwezo wa kukupatia hilo, pia, kwa hiyo afadhali umwulize mchungaji.”

⁵⁰ Basi baada ya mahubiri, wakamwuliza mchungaji. Naye mchungaji akasema, “La, mwanangu.” Kasema, “Hakuna mtu anayeweza kumwona Mungu.” Kasema, “Mungu ni kama tu hewa, wala huwezi kumwona.” Na, kwa hiyo, hakika, hilo halikumridhisha maskini huyo mvulana.

⁵¹ Naye alikuwa akijenga urafiki na mzee mmoja huko chini kwenye Mto Ohio. Naye alikuwa ni mzee mvuvi wa kawaida, mvi kichwani mwake, na yuna umri wa miaka sitini na mitano, sabini, inalundikana, akiishi kwenye mashua mbovu-mbovu. Nami nimevua samaki pamoja naye, mimi mwenyewe, nasi tulikuwa tukipanda visiwani na kuvua samaki, kuweka nyugwe zitetemekazo. Kwa hiyo maskini huyu mvulana alikuwa pamoja naye siku moja, huko juu mtoni. Ndipo walipokuwa njiani wakirudi, kulitokea dhoruba nao ikawabidi kukimbia upesi ufukoni, kutoa huo mtumbwi mdogo majini, kwa sababu mawimbi yalikuwa ni makubwa mno na yanarusha mawimbi meupe, mpaka yangeweza kuupindua maskini huo mtumbwi.

Kwa hiyo baada ya dhoruba kwisha, nao wametoka nyuma ya miti, walisukuma maskini mtumbwi huo kutoka ufukoni, nao wakaingia kwenye mkondo wa mto, ambao ulikuwa na upana wa yapata maili moja kuukingama mto Ohio kule. Wakaanza kwenda chini ya mto, wakielea, wakati huyo mzee mvuvi akivuta makasia.

⁵² Ndipo wakati wakiwa nyuma ya mti, huyo mzee mvuvi alikuwa amemwambia maskini kijana huyo hadithi (kwa kuwa alikuwa amemwuliza) ni kwa nini hakuwa ameo, wala hakuwa na mtu wa kumhudumia. Naye akasema, “Loo, mwanangu, kuna mtu Fulani anayenihudumia. Na sababu ya mimi kutokuwa, mke wangu yuko Mbinguni, akingojea.” Naye akaendelea na hiyo hadithi.

⁵³ Ndipo alipoingia kwenye mkondo wa maji, walikuwa wakienda mashariki kwa maskini mtumbwi huo...ama wakienda magharibi, hasa, pamoja na maskini mtumbwi huo, naye huyo mzee mvuvi akielekea...huko nyuma ya mto kuelekea magharibi, ilikuwa ni alasiri, na—na jua lilikuwa likitua. Na, baada ya mvua, ukatokea upinde wa mvua.

⁵⁴ Na, loo, nafikiri huo ni wakati mzuri sana! Wakati mvua imefagilia mbali uchafu wote kutoka mitini, na—nayo inaonekana mizuri sana, chanikibichi, katika rangi zao za asili. Nayo maua yote yanapendeza na halanga imeshuka, na inatoa harufu ya waridi. Ni wakati wa kupendeza tu, baada ya mvua.

⁵⁵ Nafikiri kwa namna fulani inanikumbusha, baada ya uamsho, wakati Roho Mtakatifu ameingia na kusafisha mavumbi yote, na—na kutufanya watamu tena mbele za Bwana. Kusimama tu katika Uwepo wa...kama nilivyo alasiri ya leo, nikiogelea tu hapa katika Uwepo wa Bwana Yesu. Roho Mtakatifu akiondoa tashwishi zote na hofu na kadhalika kutoka kwetu, nasi tunasimama pamoja, baada ya ma—manyunyuyu kutoka Mbinguni kuzijaza nafsi zetu.

⁵⁶ Wakati huyo mzee mvuvi alipoanza kuvuta mtumbwi wake, jamaa huyo mdogo akaona kwamba machozi yalianza kushuka kwenye uso wa huyo mzee mvuvi. Ndipo maskini mvulana huyo akageuka kuona kile alichokuwa akiangalia, na kulikuwa na upinde wa mvua angani. Kwa hiyo huyo jamaa mdogo akiketi kwenye shetri ya huo mtumbwi, akasisimka. Kwa hiyo alikuwa ameshikilia upande wa demani, ndipo akasimama, kisha akakimbia kwenye shetri ya huo mtumbwi na kuanguka kwenye mapaja ya mzee mvuvi. Naye akasema, “Nataka kukuuliza jambo fulani ambalo si mama wala mwalimu wangu wa Shule ya Jumapili, wala mchungaji, anaweza kunijibu.”

⁵⁷ Basi huyo mzee mvuvi akaacha kupiga makasia, na kusema, “Ni nini, mvulana?”

58 Akasema, “Niliona ukiangalia upinde ule wa mvua.” Kasema, “Wananiambia ya kwamba Mungu aliuweka huo huko juu.”

Akasema, “Hiyo ni kweli, mwanangu.”

Akasema, “Iwapo Mungu ni mkuu hivyo, mtu yeyote anaweza kumwona?”

59 Ndipo huyo mzee mvuvi akamkumbatia huyo mvulana mdogo kifuani mwake, na akasema, “Ubarikiwe, maskini mwanangu! Hebu nikwambie jambo fulani. Yote ambayo nimeona kwa miaka hamsini iliyopita yamekuwa ni Mungu.”

60 Kulikuwako na Mungu kwa wingi sana upande wa ndani, mpaka angeweza kumwona Yeye upande wa nje. Sasa, hiyo ndiyo njia pekee utakayoweza kumwona Mungu, ni kumwingiza ndani yako, uache Yeye aangalie kupitia macho yako, Naye atajitangaza Mwenyewe.

61 Bila shaka, Mungu yuko katika ulimwengu Wake. Hakuna mtu aliye na akili zake timamu angeweza kuwazia... Hebu shuka uende hapa chini Los Angeles, Mlima Palomar, mahali fulani, na uangalie hiyo, hizo picha ambazo wamepiga. Na mnara huo mkuu wa kuchungulia, mahali ambapo miaka milioni mia moja na ishirini ya anga ya nuru, unaweza kuona. Gawa hiyo katika maili, uone mahali ungeenda. Mbona, ungeweza kuchora safu ya tisa-tisa kuuzunguka mji huu, ungali usingeweza kuzigawa katika maili. Lakini kupita hapo kungali kuna mifumo ya jua, kupita hapo! Basi wakati mtu anapoangalia hilo, kuna jambo moja tu unaloweza kufanya, ni kuinua mikono yako na, “Jinsi,” uimbe, “Jinsi Wewe ulivyo mkuu! Jinsi Wewe ulivyo mkuu!” Kila moja likizunguka kikamilifu, mpaka wanaweza kukwambia kupatwa kwa jua na kwa mwezi, miaka ishirini kabla hakujatukia, kufikia kwa dakika moja. Limepimiwa wakati kikamilifu na Mungu!

62 Halafu kama utaangalia tu katika maumbile, jinsi ambavyo Mungu atatenda kazi miongoni mwa ulimwengu Wake. Jinsi ambavyo ulimwengu umeinama kidogo tu, upate kuleta hewa ya joto na ya baridi pamoja, kusababisha mvua inayoyatia maji mazao yako. Jinsi ambavyo Mungu anaishi katika ulimwengu Wake! Mnaamini hilo? Hakika, Yeye anaishi.

63 Basi siku moja nilikuwa nikizungumza na mtu fulani, juu ya somo la Mungu. Na ilikuwa ni huko chini, huko Kentucky. Naye akaniambia... Yeye alikuwa ni kafiri. Mimi na Bw. Wood tulikuwa tukiwinda kuchakulo, nasi tukaenda huko na kuomba kama tungeweza kuwinda kwenye eneo lake. Naye akasema, “Loo, endeleeni,” akasema.

64 Ndugu Wood akasema, “Hii ni mimi na m—mchungaji wangu, anataka kuwinda.”

⁶⁵ Akasema, “Wood, unamaanisha umekuwa duni sana hata inakubidi kumbeba mhubiri wakati wote?”

⁶⁶ Naye akasema, “La, huyu ni mchungaji wangu tu.” Kasema, “Anapenda kuwinda.” Ndipo kasema mimi. . .

⁶⁷ Nami nilikuwa nimepiga kambi huko nje kwa yapata majuma mawili, huku nina ndevu ndefu karibu nusu inchi; na—na mchafu kupindukia, kutokana na kulala chini ardhini, jinsi tulivyokuwa tukipiga kambi. Nilikuwa huko nje, nikipumzika. Na hiyo ndiyo njia yangu ya kupumzika, kwa sababu nilimkuta Mungu katika maumbile. Hiyo ilikuwa ndiyo Biblia yangu ya kwanza, ilikuwa ni Mungu katika maumbile Yake, katika ulimwengu Wake.

⁶⁸ Naye akasema, “Vema,” akasema, “ni sawa nadhani, kushirikiana na wahubiri.” Akasema, “Lakini, unajua, ninalo wazo langu la mambo hayo.” Akasema, “Siamini katika aina yoyote ya dini.” Na kulikuwako na mtu mwingine aliyekuwa ameketi pamoja naye. Ba—basi tukaendelea, kuzungumza juu ya dini (wao waliizungumzia) kwa kitambo kidogo. Nami nikasimama tu pale, nikila tofaa nililookota chini.

⁶⁹ Naye, mzee huyu aliyedhaniwa kuwa ni kafiri, akasema, “Mara nyingi nimeshangaa. Ningetaka kukutana na mhubiri mmoja.” Naye akasema, “Huyo ni yule aliyekuwa hapa Acton, wakati ule.” Akasema, “Unajua, maskini yule dada mzee huku kilimani; siwezi kulikumbuka jina lake sasa hivi.” Kasema, “Mtu huyo alikuwa amesimama kule kwenye Uwanja wa Kambi wa Methodisti,” uliodhaminiwa na kanisa la Methodisti. Hilo ni ajabu, bali lilitukia. Nasi tulikuwa tukifanya uamsho wa uponyaji.

⁷⁰ Sasa, ninyi Wamethodisti mnapaswa kuamini huo. John Wesley aliuamini. Hakika, aliuamini. Watengenezaji wote wa mwanzoni waliamini katika uponyaji wa Kiungu.

⁷¹ “Basi,” akasema, “akisimama mkutanoni usiku huo, yeye alinena na dada wa mwanamke huyu mzee huku. Ambapo mimi na mke wangu na mumewe, yote tungaliweza kufanya (alikuwa mahututi sana kwa kansa, madaktari walikuwa wamemkatia tamaa, majuma kadha hapo kabla), na kumweka kwenye maliwato ya kitandani asubuhi hiyo.” Kasema, “Yeye alikuwa mahututi sana!” Kisha kasema, “Dada yake alihudhuria mkutano huo. Naye mhubiri huyu akalitaja jina la mwanamke huyu, naye akamwambia aje, ‘aweke lesa juu ya mwanamke huyu mwenye kansa,’ dada yake. Naye akaiweka, usiku huo. Ndipo kesho yake asubuhi, akala hemu na mayai, na kupika kiamshakinywa cha sambusa za matofaa, na kukila.” Akasema, “Ninataka kukutana na mhubiri huyo siku moja.” Nikasimama hapo tu.

Nami nikasema, “Ungemjua huyo mhubiri?”

⁷² Akasema, “La, simjui.” Ndipo Ndugu Wood akaniangalia, akanikonyezea jicho.

⁷³ Nami nikasema, “Kwani unataka kuniambia huamini ya kwamba Mungu yupo?”

Akasema, “Nisingeamini isipokuwa niweze kumwona.”

Nikasema, “Mtofaa huo una umri gani?”

“Loo,” akasema, “Niliupanda hapo yapata miaka arobaini iliyopita.”

⁷⁴ Nikasema, “Ni mwanzoni tu mwa Septemba, hatujawa na hali baridi ya hewa wala chochote kile. Niambie, bwana, ni kitu gani kinachonena, ni Akili gani inayouambia huo mti na kuufanya utomvu huo uingie kwenye mizizi na kujificha kwa ajili ya kipupwe? Hebu mwaga maji juu ya kisiki uone kama yatafanya hivyo, ama uweke karai nzima juu yake, uone kama yatashuka chini na kujificha ardhini, yakikwepa hali baridi ya hewa. Kama haukufanya hivyo, hiyo hali baridi ya hewa ingeuua huo mti mara moja. Lakini Akili fulani huushusha huo utomvu chini ardhini, kutoka kwenye mti huo, na kuupasha joto; kutoka kwenye majani, yaliyoanguka ardhini, kutoka kwenye huo mti. Ndipo kwenye msimu ujao wa kuchipusha majani, kabla hata hali ya hewa haijaanza kupungua, huu hapa utomvu unapanda juu, ukileta uhai mpya. Nielezee hilo. Niambie ni kitu gani kinachosababisha hilo.”

Akasema, “Sijapata kuwazia hilo awali.”

⁷⁵ Nikasema, “Ni Mungu katika ulimwengu Wake. Mungu huwekea kila kitu wakati vizuri kabisa.”

Akasema, “Jina lako ni nani?”

Nikasema, “Mimi ni Ndugu Branham.”

⁷⁶ Akasema, “Huyo ndiye yule mtu, jina—jina la yule mtu aliyekuwa kule.”

Nikasema, “Hiyo ni kweli.”

⁷⁷ Akasema, “Pamoja na hayo masharubu yote, na kufunikwa na damu ya kuchakulo, ati ni wewe?”

Nikasema, “Huyo ndiye, mimi, mimi ndiye huyo mtu.”

Akasema, “Ulimjuaje mwanamke huyo?”

Nikasema, “Sikumjua.”

⁷⁸ “Ulijuaje atapona?” Kasema, “Alipitia tu barabarani hapa, yeye na mumewe, muda mfupi uliopita, wakitembea.”

Nikasema, “Sikujua hilo.”

Kasema, “Ulimponya?”

⁷⁹ Nikasema, “La, bwana. Mungu alionyesha hilo, Mungu alimponya, ni neema Yake ya ajabu!”

⁸⁰ Alikuwa akila tofaa, basi akaliuma. Kisha akakigeuza kichwa chake, kasema, “Mnaweza kwenda mkawinde kuchakulo.”

⁸¹ Nikaangalia kote, nayo machozi yalikuwa yakitiririka mashavuni mwake. Nikamkumbatia kwa mkono wangu, nikasema, “Ndugu, unamwamini Yeye, sivyo?” Akakitikisa kichwa chake namna *hiyo*, kisha akageuka akaenda kwenye kitalu. Loo, Mungu yuko katika ulimwengu Wake!

⁸² Siku moja, kafiri mmoja alipita nchini, miaka kadhaa iliyopita, miaka arobaini, hamsini, sitini iliyopita, akiwatafuta waongofu. Loo, alikuwa mwerevu sana pamoja na usomi wake mpaka wahubiri wa kisasa, tukinena kiakili, wasingeweza kumstahimili. Naye akawaingiza watu katika ukafiri. Basi wakati mmoja afya yake ilizorota; akapanda kwenda Colorado, karibu na ranchi ambamo nilikuwa nikiranchi na kufanya kazi. Naye alikuwa amechukua likizo nyuma huko. Mtu niliyemfahamu, naye baba yake, alikuwa ame—amejikakamua, kupiga kambi yake. Basi siku moja alikuwa anarudi kwa miguu, ndipo akasimama. Naye akaiangalia hiyo miamba, akasema, “Kwani mlitoka wapi? Mlifikaje hapo?” Nao upepo ukaanza kuvuma. Akasema, “Kwani nimekuwa makosani wakati huu wote? Iwapo kuna Mungu, hebu na anene nami!”

⁸³ Hapo, kafiri huyo ambaye wahubiri ama hamna mtu angeweza—angeweza kumzuia ama kumstahimili, hasa, katika maneno ya hekima yake, bali walimwogopa. Lakini Biblia ilisema, “Wakinyamaza, mawe yatapaza sauti mara moja.” Mungu anayo njia ya kufanya mambo. Hayo mawe yalipaza sauti! Hapo magotini mwake, huku ameinamisha uso wake ardhini, akaisalimisha roho yake ya kikafiri kwa Mungu, naye akawa Mkristo mtamu, mnyenyekevu. “Wakinyamaza, maumbile yatapiga makelele.”

⁸⁴ Mimi, mimi ni mwindaji. Na—napenda kuwinda, kwa sababu hapo ndipo nilipomkuta Mungu, kwanza, ilikuwa ni misituni. Wakati nilipotaka kumtumikia kwa mara ya kwanza, sikujua kuomba. Nasi kamwe hatukwenda kanisani; ukoo wetu, huko nyuma, walikuwa... mimi, walikuwa ni Wakatoliki. Hawakuninii... Waairishi, asili yao, mama na baba, wote wawili; isipokuwa, babu yangu alikuwa ni Mhindi. Halafu wao... Sikujua jinsi ya kuomba. Nami nilitaka kuokoka, na, mnajua nililofanya kwanza? Niliketi chini na kumwandikia Mungu barua, na kumwambia nilisikitika kwa yale niliyokuwa nimefanya. Nami nilikuwa niende huko nje mwituni, kwenye njia ya miguu ambapo nilikuwa nikishikwa na hisia ya ajabu ajabu wakati ningepitia mahali hapa, nami nilikuwa nikienda kuibandika mtini kusudi aweze kuisoma wakati akipitia hapo. Maana, nilijua Yeye aliishi huko nje misituni mahali fulani. Nilikuwa nimeona mambo mengi kupita kiasi yakitendeka; nilijua ya kwamba Yeye aliishi mahali fulani. Nami nikawazia,

“Yeye, akiwa huru sana na dhambi, angekuwa huko mahali fulani ambapo palikuwa ni safi, na pasipokuwa na watu.” Yeye angeweza... Ningempata kule vizuri zaidi kuliko nilivyoweza miongoni mwa mahali ambapo watu walikuwa wamepachafua. Nilisoma, Biblia yangu ya kwanza ilikuwa kutoka kwenye maumbile.

⁸⁵ Ama, he—hebu wachukue maskini bata hawa. Wanatoka Kusini huku, nao wanaenda, huko juu kabisa Canada, nao wanatengeneza kiota chao kule juu katika kinamasi. Nao wanataga mayai yao, nao makinda wa bata wanazaliwa. Na, halafu, hiyo ni katika msimu wa kuchipua. Mwaka huo, wanawalea, wanalishwa msimu wote wa kiangazi. Kisha kipupwe kinapoingia, mara ya kwanza kunapotokea upepo baridi ukivuma kupitia milimani, ambapo pana jalidi, inayopitia kwenye nchi ya uwanda mpana wa nyasi ambako kuna maziwa, ama safu za milima, nao upepo huo mwanana wa kwanza baridi unapopitia pale, wenye jalidi; mahali fulani katika kundi hilo kubwa la mabata kwenye dimbwi hili, kunaye maskini kiongozi mmoja, maskini bata dume. Atakimbia moja kwa moja kule nje katikati ya dimbwi hilo, ainue maskini domo hilo juu hewani, na kulia mara nne ama tano, kila bata kwenye hilo dimbwi atamjia. Atainuka kutoka hapo. Kamwe hajawahi kuwa nje ya dimbwi hilo; alizaliwa humo kwenye msimu huo wa kuchipua. Ataruka juu kutoka kwenye dimbwi hilo na kwenda moja kwa moja hadi Louisiana awezavyo kwenda, kwenye yale mashamba ya mpunga; hana dira hata kidogo. Wanaiita “silika.”

⁸⁶ Mara nyingi nimewazia, kama Mungu alimpa bata akili ya kutosha, inayoitwa “silika,” kumwongoza kutoka kwenye shida, Yeye anapaswa kufanya nini kwa kanisa lililozaliwa mara ya pili, lililojazwa na Roho Mtakatifu? Yeye anapaswa kufanya nini? Hana dira, lakini alizaliwa kiongozi! Mabata wanamjua kiongozi wao, lakini kanisa halimjui. Roho Mtakatifu ndiye Kiongozi wetu, Yeye ndiye Mwalimu wetu, atatuongoza katika Kweli, katika Uzima. Mabata wanamjua wao, bali inaonekana kana kwamba wakati mwingine hatuna akili nyingi kama aliyo nayo bata. Maana, yeye anapenda kuendelea kukaa na kile alichopewa, bali sisi hujaribu kuwazia jambo tofauti. Hiyo ni kiakili, unatoka nje ya ulimwengu mkuu wa Mungu.

⁸⁷ Nitawaambia kile mnachoweza kufanya, baadhi yenu watu kutoka kwenye nchi za baridi. Hebu mwangalie huyo nguruwe jike akienda huko kutoka upande wa kaskazini mwa kilima, na kuleta hayo magugu na mabunzi kwenye upande wa kusini wa kilima, na kutengeneza kitanda chake. Kisha usiku huo usikilize habari, nazo hizo habari zitasema, “Kesho, hali ya anga itakuwa shwari,” usisikilize hata kidogo yale asemayo. Maskini huyo nguruwe jike anajua mengi kuhusu hali ya hewa kuliko huyo atakavyowahi kujua. Hiyo ni kweli kabisa. Alienda upande wa kusini ambako kutakuwa na joto kiasi.

⁸⁸ Ukienda kuwinda sungura na uwaone hao sungura wameketi chini ya kichaka, namna *hii*, tarajia hali baridi ya hewa! Kisha ukiwaona wameingia kwenye shamba la mahindi, inakaribia kunyesha.

⁸⁹ Mwangalieni tu Mungu, Yeye hutenda kazi, loo, jinsi alivyo wa ajabu! Kama tu utayafungua macho yako, unaweza kumwona kote karibu nawe. Yeye yuko katika ulimwengu Wake, kila mahali, akitenda kazi. Mwangalie katika machweo ya jua. Mwangalie katika mapambazuko. Mwangalie katika upinde wa mvua. Mwangalie kila mahali. Unaweza kumwona, Yeye hayuko mbali sana kutoka kwako kuliko mkono wako wa kulia ulivyo. Mungu yuko katika ulimwengu Wake.

⁹⁰ Miaka kadhaa iliyopita, nilikuwa nikiwinda kulungu, huko Colorado ambako mimi huwinda sana. Basi huko juu milimani kule, ilikuwa mapema kwenye msimu wa kupukutika, wala theluji haikuwa imeanguka kwa kilindi vya kutosha kuwafanya kulungu wahame misitu ya juu, waingie chini bondeni. Kwa hiyo mimi na Jeff, yule mfugaji, tulikuwa . . . Nimemsaidia sana kuhudumia ranchi mle ndani kwa miaka kadhaa, na ningali ninawasaidia kuwakusanya ng'ombe. Nasi tulikuwa tumepanda kwa farasi, kuwinda, naye angeniacha kwa siku tatu ama nne. Alirudi kwenye mkondo wa magharibi wa Mto Troublesome, nami nilikuwa nikiwinda kwenye mkondo wa mashariki. Basi kama tungepata kulungu, tungewatundika juu, na kujua mahali pa kuwaleta farasi wa mizigo, nasi tulikuwa tu juu ya farasi wetu wa matandiko.

⁹¹ Basi siku moja nilikuwa huko juu sana, nikawaacha farasi wangu wa matandiko kwa mbali sana, nikapanda juu ukingoni. Na mwishoni mwa msimu wa kupukutika, itaninii, muda si muda mwajua, jua litakuwa likiwaka, kisha itanyesha, halafu kutatakata, halafu theluji itaingia. Na, ni hali tu ya hewa inayobadilika. Basi nilikuwa nikiwinda huko juu. Kulikuwa kumekauka sana, nami nikasikia mngurumo wa radi; ndipo nikaangalia, ikivuka milima, nayo mvua ilikuwa inakuja. Kwa hivyo, niliingia tu nyuma ya mti na kusimama pale kidogo mpaka dhoruba ikaisha. Upepo ulivuma na kupinduka, na kunyonganyonga, nami nikasimama nyuma ya miti hata ikaisha. Baada ya kumalizika . . .

⁹² Nilikuwa nimesimama pale, nikiwaza juu ya Mungu. Imekuwa ni miaka michache tu iliyopita, nilikuwa nikifanya miamsho hii. Basi nikawazia, "Jinsi Mungu alivyo mkuu, na jinsi alivyo wa ajabu!" Nikasema, "Hapana shaka nilizaliwa kwa ajili ya mahali hapa, huko misituni, nikiwa peke yangu, mbali na watu na umati, na wagonjwa na wanaoteseka, na kila kitu, simu zikilia, na magari ya kuchukulia wagonjwa yakija." Nikawazia, "Jinsi palivyo patamu na patulivu! Bwana, nijalie nikae hapa. Nami ni—nilizaliwa kwa ajili ya hapa, hii ndiyo asili yangu, hapa ni nyumbani. Hapa ndipo Wewe unapoishi." Kisha nikawazia,

“Vema, nisipoipata katika huu, nitaipata katika ule Utawala wa Miaka Elfu, kwa hiyo nitaungojea tu wakati huo.”

⁹³ Ndipo dhoruba ilipoisha, kidogo nilitoka nyuma ya huo mti. Na, kule nyuma kabisa kando ya huo mlima, nikamsikia kulungu dume mkongwe akianza ku—kulia. Naye alikuwa akiliita hilo kundi lingine; walitawanyika, wakati wa ile dhoruba. Basi akaanza kumwita mwenziwe. Ndipo kama Daudi alivyosema katika Maandiko, “Kilindi kinapoita Kilindi!” Ikiwa kuna kilindi, kinachoita, hapana budi kuwe na Kilindi cha kukiitikia, mahali fulani.

⁹⁴ Ndipo basi asili hiyo ikaanza kupanda ndani yangu. “Hapa ndipo mahali pangu pa kukaa. Loo, huo ni muziki!” Nyuma kabisa hapa, maskini mbwa mwitu wa kijivu akalia vikali, ndipo mwenziwe akamjibu, huko chini kabisa. Loo, jamani! Hapo ndipo kilindi kweli kinapoita Kilindi; kusikia wito huo wa mwitu wa mbwa mwitu, baadhi ya wanyama mwitu wakipiga kelele, ndege wanapiga kelele. Kwangu mimi, ni Mungu! Naweza kumsikia kati ya hayawani Wake na wanyama Wake.

⁹⁵ Upepo ukivuma, ilitokea nilitazama nyuma hapa ambapo . . . kuvuma, baridi vya kutosha kugandisha maji kwenye miti isiyokauka. Jua likachomoza, huko magharibi, *hivi*, na likaonekana kama jicho linalochungulia huko, kama Mungu, katika machweo ya jua. Ndipo nikagundua ilisababisha upinde wa mvua kupitia kwenye korongo kubwa. Ndipo nikaanza kuwazia, “Huyo hapo kwenye upinde wa mvua. Huyo hapo kule ng’ambo, katika mwito wa kulungu yule. Yule pale kule katika wito wa mbwa mwitu, akiita. Huyu hapa kwenye miti. Naweza kusikia sauti Yake ikinong’oneza. Huyo hapo kwenye upinde wa mvua.”

⁹⁶ Kwa maana, “Alionekana mithili ya jiwe la Yaspi na Akiki, akiwa na upinde wa mvua juu ya kichwa Chake; Alfa, Omega, mwanzo na mwisho; Yeye Aliyekuwako, Ambaye Yuko, na Atakayekuja; Shina na Mzao wa Daudi.” Na akiwa na upinde wa mvua, rangi saba, ukamilifu. Mungu hukamilika katika saba. Na huyo hapo kama upinde wa mvua pia, kama agano.

⁹⁷ Kila mahali unapoangalia, unaweza kumwona Mungu, ikiwa utaangalia tu katika maumbile Yake. Basi wakati nilipojaa kabisa . . . Nitawaambia kitu fulani, ndipo mtajua mimi ni—mimi ni Mbaptisti halisi. Wakati nilipokuwa nikitazama hayo, nilijazwa sana na Roho Mtakatifu mpaka nikaiegemeza bunduki yangu kwenye mti kisha nikauzunguka-zunguka huo mti mbio kadiri nilivyoweza, nikirusha mguu mmoja hewani, na kupiga kelele kwa sauti yangu yote, nikipiga mayowe, “Haleluya! Haleluya! Haleluya! Haleluya,” kuzunguka tu, tena, na tena, na tena, hata nusura nianguke chini; kisha nikasimama na kuikutua mikono yangu juu-chini, na hapo nikipiga mayowe, “Utukufu! Utukufu! Utukufu! Utukufu! Utukufu! Haleluya!

Haleluya! Haleluya! Haleluya,” kwa nguvu tu nilivyoweza. Nisingeweza kufikiria kitu kingine chochote cha kusema. Moyo wangu ulikuwa ukibubujika.

⁹⁸ Ilikuwa nini? Kilindi kikiita Kilindi! Nikamsikia Mungu huko nje kwa njia ambayo labda usingemsikia. Lakini, kwangu mimi, Yeye alikuwa katika ulimwengu Wake, akiniita tena, “Mimi ni Mungu wa uumbaji. Niliumba vitu vyote kwa mkono Wangu Mwenyewe.”

⁹⁹ Naam, ikiwa mtu angekuja msituni, wangefikiria walikuwa na mwendawazimu msituni. Nikauzunguka ule mti, tena, na tena, na tena, na tena, nikiwa tu na wakati mzuri sana! Sikuwa . . . mtu yeyote, sikujali kama walisikia, au la. Nilikuwa maili hamsini, maili thelathini, kwa vyovyote vile, kutoka kwa mtu yeyote, kadiri nilivyojua. Lakini nikauzunguka ule mti tena na tena, nikipiga mayowe.

¹⁰⁰ Kwa sababu gani? Nilikuwa katika kanisa kuu la Mungu. Niliweza kumwona kila mahali, jua, michirizi ikipitia msituni, ule upinde wa mvua huko ng’ambo, mbwa mwitu akipiga kelele, kulungu akipiga kelele. Ningeweza kumsikia katika upepo. Loo, jamani, Yuko kila mahali! Huko juu kabisa, ungeweza kuona mahali theluji ilipoifunika hiyo milima, na ikiweka uvuli kwenye miti isiyokauka. Loo, angalia tu mahali popote, utamwona. Yuko katika ulimwengu Wake. Mnaamini hilo? Nilisimama pale kidogo.

¹⁰¹ Ndipo baada ya kitambo kidogo nikasikia kitu fulani kikifanya, “Kwe, kwe, kwe, kwe! Kwe, kwe, kwe!”

Nikawazia, “Ni kitu gani hicho?”

¹⁰² Nikaangalia kote. Kulikuwa na uwazi pale ambapo dho—dhoruba ya awali ilikuwa imeangusha baadhi ya miti, na kulikuwako na maskini kuchakulo wa misonobari. Sijui kama mnajua hao ni akina nani, au la. Ni wangapi wanaojua kuchakulo wa misonobari ni nani? Yeye ndiye jamaa mdogo mwenye kelele nyingi sana aliyeko nchini. Naye akaruka juu ya kisiki cha zamani cha mti hapo. Naye alikuwa akifanya kana kwamba alikuwa karibu kuninii . . . alikuwa akitaka kunirarua vipande vipande, akifanya tu, “Kwe, kwe, kwe, kwe!” Alikuwa akiruka-ruka, akitetemeka mwili mzima, kwa nguvu alivyoweza. Loo, alitaka kunikata-kata.

¹⁰³ Vema, niliwazia, “Jamaa mdogo, hakuna haja ya wewe kusesimkwa hivyo. Hatafanya chochote. Nami, je, vipi, kwani nilikutisha?” Nikawazia, “Vema, hupaswi kuogopa hilo. Nilikuwa tu nikimsifu Mungu aliyetumba sote wawili.” Unaona? “Huna haja kuvurugika hivyo. Nilikuwa nikimsifu Yeye, kwa hivyo usisisimkwe hivyo. Vema, nilikuwa tu nikimsifu Mungu, ulipaswa kujua vema zaidi kuliko kunipigia kelele namna hiyo. Usinisumbue wakati nikipiga kelele namna hiyo, kwa sababu nina wakati mzuri. Achana na mimi.” Unaona?

104 Na kwa hivyo ikawa niliona yule jamaa mdogo angetupa kichwa chake upande, na kuangalia chini kwenye hicho kichaka. Vema, nikaona kwamba hakuwa akinibwekea. Kutoka kwenye kichaka hicho, kwenye ile dhoruba, kulikuwa na tai mkubwa aliyelazimika kushuka chini. Na alikuwa amesukumiwa mle ndani ya huo, alishushwa chini katika uwazi huo. Na huyo jamaa mkubwa, huyo ndiye aliyemfanya maskini huyo kuchakulo kususimkwa hivyo. Naye akaruka juu ya tawi.

105 Nikawazia, “Sasa, subiri kidogo hapa, kuna kitu fulani mahali fulani. Kwa sababu, nilikuwa nikimwabudu Mungu, nikikimbia kuuzunguka-zunguka mti huu hapa. Nami ninamwona katika elementi hizi Zake zote mbalimbali, na maumbile haya. Sasa, kwa nini anikatishe kwa ajili ya kitu kama hicho?” Sasa, kulikuwa na maskini tai. Ninampenda tai. Lakini nilimwangalia, ndipo nikawaza, “Vema, ni nini... Je, ningeweza kumwona Mungu ndani yake? Sasa hiyo ingekuwa nini?”

106 Nikamwangalia. Macho yake makubwa mno, yaliyoonekana ya kijivu, naye alisimama pale kwenye tawi hilo, akinitazama. Ndipo akamwangalia kuchakulo huyu, kisha akageuka akaniangalia; halafu akamwangalia huyo kuchakulo, akamwangalia. Nikasema, “Nadhani unatutazama.” Kwa hiyo nikawazia, “Unajua nini? Ningeweza kukupiga risasi, kama nilitaka.” Nami nikamwangalia. Nayo bunduki yangu ilikuwa imeegemezwa kwenye mti. Nikasema, “Je, ulijua ningeweza kukupiga risasi kama ningetaka?” Kamwe hakujali hilo, ameketi tu pale.

107 Nikawazia, “Loo, hilo ndilo Mungu anataka nione, ‘Usiogope.’” Huyo tai ni jasiri, haogopi chochote. Asingeona aibu kumwambia bosi wake alikuwa ameponywa kwa uponyaji wa Kiungu. Haitamsumbua. Yeye ana—ana nguvu. Hangeogopa kutoa ushuhuda ikiwa alikuwa amepokea Roho Mtakatifu. Kama alikuwa ni kwa ajili yake, hakika angemshuhudia; maana yeye ni jasiri, hakuna cha kumtia aibu.

108 “Vema,” nikawazia, “una ujasiri hivi kwa nini? Ni nini kinachokufanya uwe jasiri?” Nikaanza kuona basi, aliendelea kuhisi mabawa hayo. Mnajua jinsi wanavyosogeza manyoya yao nyuma na mbele, mnajua, kuvuta mabawa yao. Nikawazia, “Loo, kumbe. Uh-huh. Mungu alikupa mabawa mawili. Nawe unajua vizuri sana kwamba ungeweza kuchukua hayo mabawa mawili makubwa na kuingia kwenye msitu ule kabla hata sijaweza kuifikia ile bunduki.” Alikuwa na imani na yale... Mungu alimpa hayo mabawa, naye alijua kile hayo mabawa yangeweza kumfanyia.

109 Ni tofauti jinsi gani na mwanadamu! Mungu alitupatia Roho Mtakatifu, na bado hatujui yale atakayotufanyia. Hiyo ni kweli! Hayana kikomo, yale atakayofanya. “Yoyote myatakayo,

mkiomba, aminini mtayapokea, nayo yatakuwa yenu.” Tai huyo angeweza kutumainia mabawa yake aliyopewa na Mungu. Mnajua ni kwa nini? Nafikiri, mara nyingi, huyo tai alikuwa ameyajaribu kwelikweli. Alijua alichokuwa akizungumzia. Nasi tunaye Roho Mtakatifu wala hatujamjaribu. Hapo ndipo lilipo tu. Tazama, laiti tungaliacha maumbile yatende kazi ndani yetu kama mnyama afanyavyo! Hakika, anajua cha kushikilia, na asichopaswa kushikilia.

¹¹⁰ Kwa hivyo a—alijua umbali kutoka mahali nilipokuwa nimesimama, kutoka kwenye bunduki yangu, angeweza kuwa kwenye msitu ule wala kamwe nisingeweza kumwona, kwa hivyo akaendelea kuyasogeza mabawa hayo makubwa. Nami nikamwangalia, nikasema, “Jamani wee, kamwe nisingekupiga risasi. Ninakujivunia sana!” Ninapenda kuona kitu chenye ujasiri ndani yake, kitu ambacho kitasimama wakati wanapojua wanachofanya. Hivi hampendi kuona hicho?

¹¹¹ Hiyo ndiyo sababu napenda kanisa la Pentekoste. Halijali kile ulimwengu usemacho, kuwaita “watakatifu wanaojibingirisha,” kila kitu kingine, wao husimama moja kwa moja na kupiga makelele vile vile, wanamsifu Bwana, wanaendelea moja kwa moja. Ninapenda hilo. Bila shaka, simama imara kwacho. Haileti tofauti yoyote hata iwe nani, kaa hapo na kutoa ushuhuda wako, mpe Mungu sifa.

¹¹² Nilimwangalia maskini tai huyu wakati akizunguka pale, mwajua, kidogo. Ndipo ikawa niliona, zaidi sana hakuwa akiniangalia, alikuwa akichoshwa na kumsikiliza yule kuchakulo akimlaani, “Kwe, kwe, kwe! Kwe, kwe, kwe!” Ah, alimtazama tu. Basi baada ya muda kidogo akamkasirikia, kwa hivyo, jambo pekee alilofanya ni kufanya tu mruko mkubwa namna *hiyo*, na kupigapiga mabawa yake karibu mara mbili, naye huyo alikuwa ameuvuka huo msitu. Halafu hakuyapiga mara moja zaidi, aliyatuliza tu mabawa yake. Na kila wakati hewa ingeinuka, angeinuka pamoja nayo. Nami nilisimama pale na kumtazama. Kwa kuwa kila wakati upepo ungeingia kasi, angepaa juu zaidi kidogo; kamwe hakusogeza unyoya, ni kwenda tu juu, juu, juu, juu, mpaka yeye akawa doa dogo.

¹¹³ Nilisimama pale, nayo machozi yakaanza kutiririka mashavuni mwangu. Nikasema, “Ee Mungu, hapa ni mahali pazuri sana kuwa. Hapa ndipo napenda kuwa. Wewe huyo hapo katika tai huyo.”

¹¹⁴ Mnaona, alifanya tu mruko mmoja mkubwa, naye aliyaamini mabawa yake. Hakupigapiga kutoka mkutano mmoja hadi mwingine, na kwenda kutoka kanisa moja hadi lingine. Alifanya tu mruko mmoja mkubwa, kisha akayatuliza mabawa yake katika Nguvu za Mungu, akamwachilia Roho Mtakatifu, amchukue ampeleke mbele, zaidi na zaidi, na zaidi na zaidi. Aliwaondokea kuchakulo milia hawa wa humu duniani,

wasioweza kuondoka duniani; hawana mabawa, wala hawajui kuruka. “Kwe, kwe! Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama Roho Mtakatifu, huyo ni kwa ajili ya siku nyingine iliyopita.” Loo, weka tu mabawa yako katika Nguvu za Mungu, acha Roho Mtakatifu akuinue juu yake, endelea mbele zaidi na zaidi na zaidi. Asingeweza hata kumsikia kuchakulo milia mwingine tena, kuchakulo wa ardhini, au chochote mnachotaka kumwita. Alichoshwa na hiyo “kwe, kwe.” Loo, laiti kanisa, moja ya siku hizi, litachoshwa na hayo, nao watajua jinsi ya kuweka mabawa yao; na watatembea pamoja na Mungu, waende Nyumbani, watoke huko. “Siku za miujiza zimepita”? Niambie lini. Wamekuja wamechelewa sana kutwambia hilo, sivyo? “Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama Roho Mtakatifu. Kunena kwa lugha ni udanganyifu tu,” hayo ndiyo tu wajuayo kulihusu. Kwa hivyo, jambo la kufanya ni kuweka tu mabawa yako.

¹¹⁵ Hakuruka, sasa, kutoka mahali pamoja hata pengine. “Nitaenda nione kama *hili*, na nitaenda huko nione kama *lile*.” Alijua tu jinsi ya kuweka mabawa yake. Na hayo ndiyo yote yakupasayo kujua jinsi ya kufanya juu ya Uponyaji wa Kiungu, juu ya Roho Mtakatifu, ni kujua tu jinsi ya kuweka imani yako katika nguvu na ahadi za Mungu. Itakubeba moja kwa moja juu. Utapaa tu moja kwa moja juu. Kila wakati anapovuma, tutainuka juu zaidi na zaidi, na juu zaidi na zaidi; mpaka hutaweza kusikia hii hapa, “Kwe, kwe, kwe! Siku za miujiza zimepita. Kundi la watakatifu wanaojibingirisha.” Hutalizingatia kamwe. Utakuwa mbali sana nao mpaka utakuwa umbali usioweza kuwasikia. Nafsi yako itainuliwa kufikia mahali ambapo. . .

¹¹⁶ Loo, hakika, Mungu yuko katika ulimwengu Wake. Mnaamini hilo, sivyo? Loo, tungeweza kutumia saa kadhaa kwenye jambo hilo moja tu. Hatuna budi kurukia lingine. Mnaamini Mungu yuko katika ulimwengu Wake? Sasa, pili, Mungu yuko katika Neno Lake. Sasa wewe tazama kote ulimwenguni nawe utamwona Mungu. Hakika, utamwona. Sasa Mungu yuko katika ulimwengu Wake.

¹¹⁷ Sasa, Mungu yuko katika Neno Lake. Mungu hutimiza Neno Lake. Hilo ndilo linaloifanya Biblia kuwa halisi. Hilo ndilo tunaloweza kumpa mkana-mungu yeyote changamoto, asiyeamini yeyote, Mwislamu yeyote, Mbudha yeyote, mchawi yeyote, mwanamizimu yeyote, kitu chochote kile, katika Jina la Bwana Yesu, na kulifanya Neno hili liishi, kwa sababu Mungu yuko katika Neno Lake.

¹¹⁸ Nilikuwa nikijadiliana, hivi majuzi, na—na kanisa fulani la kimadhehebu linaloamini kwamba—kwamba kanisa ndilo jibu, si Neno. Walisema waliandika Biblia. Biblia ilikuwa. . . ilikuwa historia ya kanisa lao. Kisha akasema, “Mungu yuko katika kanisa Lake.”

Nikasema, “Biblia ilisema, ‘Mungu yuko katika Neno Lake.’”

¹¹⁹ “Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu.” Hiyo ni kweli. Yeye alikuwa Neno la Mungu, Neno la Mungu lililonenwa. Naye Mungu yuko katika Neno Lake. Kila ahadi anayofanya Mungu, Yeye husimama na ahadi Yake. Jambo pekee tunalopaswa kufanya, ni, kuliingiza Neno Lake moyoni mwetu, wala tusilitilie shaka, bali tuamini, ndipo Mungu anafanya Neno hilo (ambalo ni Yeye mwenyewe ndani yako) kuingia kazini na kutimiza jambo lile lile aliloahidi.

¹²⁰ Je, alilitimiza katika Ibrahimu? Mbona, Ibrahimu, mtu mwenye umri wa miaka sitini na mitano, au, kabla hata yeye, au, umri wa miaka sabini na mitano, kabla hajapokea ile ahadi. Naye akaliiweka Neno hilo moyoni mwake na kuliweka mle muda wa miaka ishirini na mitano. Lakini lilitoa kile hasa hiyo ahadi ilichokuwa. Hiyo ni kweli?

¹²¹ Mungu yuko katika Neno Lake. Sote tunajua hilo. Hakuna hata chembe moja ya Biblia inayojipinga Yenyewe. Nimemtolea mtu yeyote kitu chochote watakacho; nitahubiri Injili na kuchukua sadaka za upendo kwa mwaka mmoja, na kuitoa, kila chembe, kwa mtu ambaye anaweza kulichukua Neno la Mungu na kulikosoa kwa Neno la Mungu, kwangu mimi. Hiyo ni kweli. Hakuna. Na nimekuwa na changamoto hiyo kwa miaka na miaka; ningali ninachukua matoleo yangu mwenyewe ya upendo. Sababu, hakuna. Unaweza ukachanganyikiwa sana katika akili zako mwenyewe, kwa sababu Biblia ni... Yesu alimshukuru Baba Yake kwa “kuificha kutoka kwa macho ya wenye hekima na akili, na kuwafunulia watoto wadogo wanaoweza kujifunza.” Mnaona, ni Neno la Mungu.

Neno ni kama Mbegu.

¹²² Sasa, hebu chukua mbegu. Ninyi watu hapa kwenye Pwani ya Magharibi, ninyi ni wakulima hodari. Sasa, chukua mchungwa wako. Sasa, chukua mchungwa wako, unapoupata kwa mara ya kwanza, ni mbegu. Hebu ipande ardhini, nayo hiyo mbegu itazaa mchungwa. Hakika. Sasa, hivyo ndivyo ilivyo. Sasa, mchungwa huu, jambo pekee unalofanya nao, wakati ukiwa mrefu tu kama ninii yako... urefu wa inchi moja. Sijui ni pishi ngapi za mchungwa mti mmoja ungetoa maishani mwake. Hebu tuseme, kwa mfano, pishi mia tano. Sasa, hiyo inaweza kuwa zaidi ama pungufu, sijui; lakini tuseme pishi mia tano. Je, unajua ya kwamba kila chungwa litakalopata kuwa kwenye mti huo liko ndani yake wakati huo ukiwa na urefu wa inchi moja? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Ulijua hilo? Hakika, ndivyo ilivyo. Wapi? Linatoka kwenye mbegu. Sasa, jambo pekee ni kwamba, umepandwa tu, ukawekwa.

¹²³ Nao hauna budi kunywa, unanyonya maji kutoka ardhini, upate lishe. Nao unanyonya maji kutoka ardhini, nao hauna budi kunywa zaidi ya kipimo chake. Na kila wakati...bila shaka, hauna budi kusukuma nje. Na unapokunywa maji, unasukuma nje matawi; unakunywa maji zaidi, unasukuma nje majani; unakunywa maji zaidi, unasukuma nje maua; unakunywa maji zaidi, unasukuma nje machungwa. Unaendelea tu kunywa, na kusukuma nje. Lakini, hauna budi kunywa.

¹²⁴ Hivyo ndivyo mwaminio alivyo, amewekwa moja kwa moja katikati ya Neno la Mungu. Amina! Na endapo ana haja na kitu chochote, yeye anakunywa tu, na kusukuma nje; anakunywa, na kusukuma nje. Mtu anapojazwa na Roho Mtakatifu, kila kitu atakachopata kutumia katika safari ya maisha yake kiko ndani yake papo hapo. Naam, bwana. Jambo pekee litupasalo kufanya ni kunywa na kunywa, na kunywa na kunywa, na kunywa mpaka tukipate. Tumepandwa katika Kristo Yesu! Na kwa tafsiri yangu Yake, Yeye ni Chemchemi ya Uzima isiyoweza kwisha. Hicho ndicho hasa ninachowazia Yeye alichu. Ndipo tunapopandwa ndani Yake, Yeye hawezi kwisha! Tunaweza kunywa kutoka Kwake, wema, upole, unyenyekevu, subira, nguvu, uponyaji, [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...ahadi anayotoa, maana sisi tumepandwa katika Mbegu ya Neno Lake. Nalo litatoa kile hasa Mungu alichosema litatoa. Ni Mbegu, Neno.

¹²⁵ Mungu yuko katika Neno Lake. Tunaamini hilo, sivyo? Sote tunaamini. Mnamwona Mungu akijibu. Miaka mingi iliyopita, wakati alipowaambia wapande juu, Pentekoste, wangempokea Roho Mtakatifu. Miaka kadhaa kabla ya hapo, katika Isaya, Yeye alisema, “Amri lazima iwe juu ya amri, kanuni juu ya kanuni, hapa kidogo na pale kidogo. Shikilia yaliyo mema. Midomo migeni na lugha zingine nitasema na watu hawa, na hii ndiyo Raha.” Mnaona, Yeye alilisema awali sana, ndipo Neno Lake likaja moja kwa moja na likadhihirishwa. Wote, Masihi aliyeahidiwa, tangu bustani ya Edeni, “ile Mbegu inapaswa kukiponda kichwa cha nyoka,” kadhalika, likatimia. Mungu yuko katika Neno Lake.

¹²⁶ Sasa, Mungu yuko katika ulimwengu Wake, semeni, “Amina,” kama mnaamini hilo. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mungu yuko katika Neno Lake. Mnaamini hilo? Semeni “Amina.” [“Amina.”]

¹²⁷ Sasa, Mungu katika Mwanawe. Sasa, Mungu alikuwa katika Mwanawe. “Mungu alikuwa katika Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake,” hivyo ndivyo Maandiko yasemavyo. Yeye, Mungu atashuka, na aliishi katika mwili, akazaliwa na bikira Mariamu, naye Mungu akajidhihirisha kupitia kwa Kristo; kuonyesha vile sifa Zake—Zake zilivyokuwa, kuonyesha ya kwamba alipenda, kuonyesha ya kwamba uvumilivu Wake, kuonyesha nguvu Zake, kujionyesha na

kujidhihirisha Mwenyewe. Mungu aliishi katika Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.

¹²⁸ Nilizungumza na mwanamke, hapa siku moja, ama aliita usikivu wangu. Akasema, “Mchungaji Branham,” akasema, “Ninapendezwa na mahubiri yako. Mimi, mimi ni... Mimi huihudhuria mikutano yako.” Lakini alikuwa ni mfuasi wa kanisa fulani la kimadhehebu lisiloamini ya kwamba Yesu alikuwa ni Mungu. Basi akasema, “Vema, Yeye hakuwa Mungu.” Nami nikasema... Kasema, “Unajaribu kumfanya Mungu kupita kiasi.”

Nikasema, “Yeye alikuwa Mungu.”

¹²⁹ “Loo,” akasema, “bwana, nitakubali ya kwamba Yeye alikuwa ni mtu mzuri.” Wala sitaki kuudhi hisia zenu; baadhi yao ni marafiki zangu wa thamani. Ni Sayansi ya Kikristo. Naye akasema, “Yeye, Yeye si Mungu.” Kasema, “Nitakubali Yeye alikuwa nabii, bali hakuwa Mungu. Nawe unajaribu kumfanya Mungu.”

¹³⁰ Nikasema, “Ama alikuwa Mungu au mdanganyifu mkubwa sana ulimwengu ulipata kuwa naye.” Hiyo ni kweli. Nikasema, “Alikuwa Mungu. Alikuwa zaidi ya nabii. Yeye alikuwa Mungu juu ya manabii! Hakika, alikuwa.” Nikasema, “Alikuwa Mungu.”

¹³¹ Ndipo akasema, “Sasa, ulisema ulikuwa wa ‘kimsingi,’ nawe uliyaamini Maandiko.”

Nikasema, “Ninayaamini.”

¹³² Naye akasema, “Kama nikikuthibitishia, kwa Biblia yako mwenyewe, ya kwamba Yeye hakuwa Mungu, utashuhudia kwamba ninasema kweli?”

¹³³ Nikasema, “Naam, bwana. Kama Biblia ilisema Yeye hakuwa Mungu, basi nitaamini Biblia.” Nami nikasema, “Lakini sina budi kuyaona hayo Maandiko.”

¹³⁴ Akasema, “Katika Yohana, kwenye Yohana Mt. lilisema, ‘Wakati Yesu aliposhuka kwenye kaburi la Lazaro, alilia.’” Kisha kasema, “Unajua, kama alikuwa Mungu, asingeweza kulia.”

Nikasema, “Dada, hapo ndipo unapowekea wazo lako msingi?”

¹³⁵ Akasema, “Naam, bwana. Na hiyo ni kweli. Yeye alienda kwenye kaburi la Lazaro, akalia; hiyo ilionyesha ya kwamba hakuwa Mungu.”

¹³⁶ Nikasema, “Hoja yako ni nyembamba kuliko mchuzi uliotengenezwa kwa kivuli cha kuku aliyekufa kwa njaa.” Nikasema, “Vema, unajua vema kuliko hivyo.”

¹³⁷ Naye akasema, “Loo, Yeye alikuwa—Yeye alikuwa—Yeye alikuwa nabii, alikuwa mtu mwema.”

¹³⁸ Nikasema, “Alikuwa ni zaidi ya... Mungu alikuwa ndani Yake. Yeye alikuwa ni mwanadamu, bali alikuwa Mtu mwe—

mwenye asili mbili. Moja, Yeye alikuwa mwanadamu; Roho iliyokuwa ndani Yake ilikuwa ni Mungu!” Nikasema, “Mungu alikuwa ndani ya Kristo.”

Akasema, “Ah! La!”

¹³⁹ Nikasema, “Angalia, mama, nitayachukua Maandiko yako yenyewe. Yeye alikuwa mwanadamu, lakini alikuwa ni Mungu-mwanadamu. Aliposhuka kwenye kaburi la Lazaro, kweli alilia kama mwanadamu. Hiyo ni kweli. Lakini wakati aliposimama pale, akayanyosha maskini mabega Yake yaliyoinama, na kusema, ‘Lazaro, njoo huku,’ naye mtu aliyekufa, aliyekuwa amekufa siku nne, akafufuka, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Mwanadamu asingeweza kufanya hivyo. Huyo alikuwa ni Mungu katika Mwanawe.”

¹⁴⁰ Alikuwa mwanadamu aliposhuka mlimani, ana njaa, akitafuta chakula, akitazama moja kwa moja mtini apate chakula. Alikuwa ni mwanadamu alipokuwa na njaa. Lakini wakati alipochukua samaki wawili na biskuti tano na kuwalisha watu elfu tano huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Huyo alikuwa ni Mungu katika Mwanawe. Hakika alikuwa hivyo!

¹⁴¹ Alikuwa ni mwanadamu wakati alipokuwa amelala huko nje kwenye mashua hiyo usiku huo, nguvu zilikuwa zimemtoka, hata akawa dhaifu sana asingeweza... mawimbi hata hayakumwamsha, akirushwarushwa kwenye maskini mashua hiyo, kama kizibo cha chupa huko kwenye bahari kuu. Wale ibilisi elfu kumi wa baharini waliapa wangemzamisha usiku huo wakati alipokuwa amelala. Alikuwa mwanadamu wakati aliposhikwa na usingizi na ni mchovu. Lakini alipouweka mguu Wake juu ya demani ya hiyo mashua, akaangalia juu na kusema, “Amani, tulia,” nazo pepo na mawimbi yakamtii, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Mungu alikuwa ndani ya Mwanawe! Kweli kabisa!

¹⁴² Alikuwa ni mwanadamu wakati alipokufa pale msalabani, akilia kwa sauti kuu apate rehema. Alikuwa ni mwanadamu hapo alipokufa. Alilia kama mwanadamu, alikuwa na uchungu kama mwanadamu. Lakini kwenye asubuhi ya Pasaka wakati alipovunja ninii... mauti, kuzimu, na mihuri ya kaburi, kisha akafufuka tena; Yeye ni zaidi ya mwanadamu, alithibitisha Yeye alikuwa ni Mungu!

Alipoishi, alinipenda; alipokufa, aliniokoa;
Alipozikwa, aliziondolea mbali dhambi zangu;
Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele;
Siku moja Yeye yuaja—loo, siku tukufu!

¹⁴³ Mungu alikuwa ndani ya Mwanawe, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Mnaamini hilo? Hakika. Mungu alikuwa ndani ya Mwanawe. Upesi, muda wetu unapita. Jambo moja zaidi. Sisi... Mnaamini Mungu yuko katika ulimwengu

Wake? Mungu yuko katika Neno Lake? Mungu alikuwa ndani ya Mwanawe?

¹⁴⁴ Sasa, Mungu katika watu Wake. Vema. Tutaona kama Yeye huwashukia wanadamu kadiri anavyoyashukia maumbile. Wanadamu ni sehemu ya maumbile Yake. Bila shaka, ndivyo walivyo. Sasa angalieni, Mungu alikuwa ndani ya watu Wake.

¹⁴⁵ Alikuwa ni nani hivi majuzi usiku kwenye somo letu, katika Eliya, wakati maskini mtoto mchanga alipokuwa amekufa kwa ugonjwa wa jua kali, naye alikuwa amelazwa saa kadha wa kadha kitandani mwa nabii, wakati mtu mmoja, aliyeitwa “Eliya,” alipotembea huku na huku, juu chini sakafuni, kisha akaulaza mwili wake juu ya mtoto huyo aliyekufa, naye akafufuka? Huyo alikuwa ni Mungu katika watu Wake. Hakika ilikuwa hivyo.

¹⁴⁶ Alikuwa ni nani, ambaye wakati Mtakatifu Petro, yule mtume, mvuvi asiye kuwa na elimu kiasi kwamba...Biblia ilisema, “Alikuwa asiye na elimu wala maarifa.” Alikuwa ni nani, wakati aliposhuka mitaani kwa miguu, nao watu wakawaweka wagonjwa kwenye kivuli cha mtu huyo, nao wakaponywa? Je, kivuli cha mtu ndicho kilichowaponya? Ilikuwa ni Mungu katika watu Wake, aliyefanya huo uponyaji.

¹⁴⁷ Alikuwa ni nani katika Mtakatifu Paulo, wakati walipochukua kutoka mwilini mwake leso na nguo, na kuziweka juu ya wagonjwa? Mungu alikuwa katika watu Wake. Walimtambua Mungu ndani ya Mtakatifu Paulo. Bila shaka, walimtambua.

¹⁴⁸ Ilikuwa ni nani wakati kundi la maskini waoga lilipoomba, likachukua Neno la Mungu kwenda hadi Pentekoste? Walikuwa wameifunga milango yote, na madirisha yameshindiliwa, nao walikuwa mle ndani siku kumi. Mara ikaja sauti kutoka Mbinguni kama upepo wa nguvu, ukienda kasi, ukaijaza nyumba waliyokuwa wameketi, ndimi zilizogawanyika zikawakalia, kama moto. Nao wakaingia mitaani, ambako wakati mmoja waliogopa, wakaenda huko nje, wakihubiri Injili na kufanya kama kundi la walevi. Ilikuwa ni kitu gani? Mungu ndani ya watu Wake. Mungu akitenda kazi miongoni mwa watu Wake.

¹⁴⁹ Mungu yuko ndani yenu. Mungu, Roho Mtakatifu, yuko ndani yenu, akitembea kote sasa, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.

¹⁵⁰ Ni kitu gani kinachowafanya hawa wahudumu waliovuviwa kuihubiri Injili? Ni kitu gani kinachowafanya? Labda, wakati mmoja, walevi; wakati mmoja, wacheza kamari; wakati mmoja, watu wabaya; mara, kitu fulani kikabadilika! Nao hawa hapa wamesimama, wakihubiri Injili na kuyatoa maisha yao. Na baadhi yao, karibu wote, wakiishi kimaskini wawezavyo. Wakati walikuwa wafanyabiashara na wangeweza kuwa matajiri, waendeshe magari makubwa na kuwa na anasa, bali walijitolea

na kutoa hayo. Kwa nini? Mungu yuko ndani ya watu Wake, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Mungu yuko ndani ya watu Wake.

¹⁵¹ Ni kitu gani kinachomgusa maskini mwanamke ama maskini mwanaume, naye anasimama, nao uso wake unang'ara kama mshumaa, na kunena kwa lugha asiyojua kitu kuihusu, na mwingine anasimama chini ya uvuvio wa namna ile ile na kutoa ujumbe kwa kanisa Lake? Mungu ndani ya watu Wake. Amina.

¹⁵² Ni kitu gani kinachokuja kwenye jukwaa hili, mkutano baada ya mkutano, na kufanya miujiza ile ile ambayo Yesu alifanya alipokuwa hapa duniani? Ni Mungu ndani ya watu Wake. Haidhuru ingekuwa ndani yangu kiasi gani, haina budi kuwa ndani yenu, pia. Kwa sababu, haitatenda kazi nikiwa peke yangu. Inahitaji mimi na wewe pamoja, apate kutenda kazi. Hiyo ni kweli.

¹⁵³ Sisi sote pamoja, Mungu ndani yetu sote! Mungu, sio tu katika Mmethodisti ama Mbaptisti, ama Mpentekoste ama Mpresbiteri, bali Mungu yuko ndani ya kila mwaminio ambaye amempokea Roho Mtakatifu. Huyu ni Mungu, Roho Mtakatifu, ndani ya watu, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.

¹⁵⁴ Angalia jinsi anavyowafanya watu waliamini. Kwa mambo yale yale aliyofanya kwa wale wa kwanza kwenye Pentekoste, Yeye anawafanyia leo hii, vile vile. Wao walimpokea Roho Mtakatifu vile vile, ishara zile zile na maajabu yanawafuata.

¹⁵⁵ Mungu yuko katika ulimwengu Wake. Mnaamini hilo? Mungu yuko katika Neno Lake. Mnaamini hilo? Mungu yuko ndani ya Mwanawe. Mnaamini hilo? Mungu yuko ndani ya watu Wake. Mnaamini hilo? Mungu akitenda kazi katika wote!

¹⁵⁶ Kwa hiyo Filipu alisema, "Utuonyeshe Baba, nayo yatutosha."

¹⁵⁷ Nimeridhika leo hii ya kwamba ninaweza kumwona Mungu kila mahali niangaliapo! Sio kwamba ninamwona tu, bali ninamhisi na kujua Yeye yuko hapa! Kama vile mshairi alivyosema, "Ati mnaniuliza jinsi ninavyojua Yeye yu hai, Yeye anaishi moyoni mwangu." Ninaangalia Roho Wake na kumwona akinipa motisha, akinisogeza. Unahamasishwa na kitu Fulani, Roho Mtakatifu. Mungu yuko hapa leo hii, enyi marafiki. Mungu yuko hapa.

¹⁵⁸ Yeye yuko katika maumbile Yake huko nje, kiangazi na baridi kali, majani, maua, ndege, wanyama. Yuko kwenye kutua kwa jua, kuchomoza kwa jua. Yuko kwenye mfumo wa jua. Yuko kila mahali! Mungu yuko kila mahali! Yuko katika ulimwengu Wake.

¹⁵⁹ Mungu yuko katika Neno Lake. Mtu yeyote atakayechukua Neno Lake, ahadi yoyote. . . Hebu niingie kwenye kumbukumbu kwa kusema hili. Kama utachukua msimamo mzuri wa kiakili

kwenye ahadi yoyote ya Kiungu ya Mungu, itatimizwa. Hivyo ndivyo ninavyowazia juu ya Neno Lake. Hebu chukua ahadi yoyote Humu ndani, kisha uchukue msimamo mzuri wa kiakili kwake, Mungu atakutimizia. Mungu yuko katika Neno Lake.

¹⁶⁰ Mungu yuko ndani ya Mwanawe. Yeye alikuwa ni Mungu. Yeye ni Mwana wa Mungu. Ninaamini hilo kwa yote yaliyo ndani yangu. Ninaliamini. Naam, bwana. Yeye hakuwa zaidi. . . . Alikuwa ni nabii. Hakika, Yeye alikuwa nabii, alikuwa mhubiri, alikuwa mwimbaji. Alikuwa—alikuwa Mungu, Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Mungu alishuka katika mwili, kuupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Ndipo huyo Mwana wa ajabu wa Mungu akafa. Basi, alipokufa, aliutoa uhai Wake. Akafufuka tena kwenye Pasaka, na Mungu akaufufua mwili Wake na kuuweka kwenye mkono Wake wa kuume, kisha akamtuma Roho Mtakatifu tena apate kuendelea kujitambulisha Mwenyewe miongoni mwa watu.

¹⁶¹ Naye Roho yuyo huyo aliyekuwa katika Yesu Kristo yuko miongoni mwetu leo hii, akiendelea kujidhihirisha Mwenyewe kwa watu, kwa ishara zile zile, maajabu yale yale, akiwapa Roho Mtakatifu yeye yule, akinena kwa lugha za namna ile ile, akitoa tafsiri ya namna ile ile, akiona maono, akitoka nje, akiwaponya wagonjwa, jinsi tu hasa Yeye alivyofanya hapo mwanzo. Mungu yuko ndani ya watu Wake!

¹⁶² Kwa nini tunaangalia basi, “Utuonyeshe Baba nayo yatutosha”? Tunamwona Baba. Tunamwona Baba.

¹⁶³ Ninapo—ninapoangalia hapa nje na kuona machweo ya jua, ninamwona Baba. Ninapoyaona mapambazuko, ninamwona Baba. Ninaposikia mwito wa mwituni wa hayawani, ninamwona Baba. Ninapoyaona maua hayo yakichanua, ninamwona Baba. Nawe je?

¹⁶⁴ Ninamwona katika Neno Lake. Kila ninapolichukua Neno Lake kwa ahadi, ninamwona Baba.

¹⁶⁵ Ninapomtazama Yesu, ninamwona Baba akijionyesha Mwenyewe kupitia Mwanawe.

¹⁶⁶ Nikiwaangalia watu Wake, ninamwona Baba; ninamwona akitenda kazi miongoni mwa watu Wake, akijionyesha Mwenyewe, akiendelea. “Unionyeshe Baba”? Huyu hapa papa hapa alasiri ya leo, akitenda kazi miongoni mwa watu Wake, ndani ya watu Wake, kupitia kwa watu Wake, juu ya watu Wake. Haleluya! Mungu yuko ndani ya watu Wake.

¹⁶⁷ Na tuombe. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Mungu asifiwe! Mnampenda? Vema.

¹⁶⁸ Ninaamini Billy aliniambia ninii hamsini za maombi. . . . Vema. Kadi ya maombi namba moja. Inua mkono wako, upesi sana, tupate kuona sasa, na tuingie upesi sana kwenye mstari wa maombi. Tutaona jambo fulani likitukia. Mimi. . . . Mnalingojea?

Kadi ya maombi namba moja, ni nani aliye nayo? Mama huyu hapa, una kadi ya maombi namba moja? Ninauliza kadi ya maombi namba moja. (I—ilikuwa ni herufi gani?) E.

¹⁶⁹ Kadi ya maombi E, namba moja, inua mkono wako. Namba mbili. Vema. Namba tatu, namba nne. Njoni papa hapa, sivyo? Namba tano, sita, saba. Hiyo ni kweli, simama moja kwa moja. Mara ninapoita, simama. Saba, nane, tisa, kumi, kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano, kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane, kumi na tisa, ishirini, ishirini na moja, ishirini na mbili, ishirini na tatu, ishirini na nne, ishirini na tano, fanyeni mstari sasa.

¹⁷⁰ Ni wangapi wasio na kadi ya maombi, inueni mikono yenu. Mnaamini Mungu yuko ndani ya watu Wake? Mungu yule yule aliyetembea Galilaya, katika Yesu Kristo, mnaamini yuko hapa leo hii, ndani yenu, Roho yule yule aliyekuwa ndani ya Yesu? Yeye ni Mwana wa Mungu aliyezaliwa na bikira; nanyi ni wana waliopewa mamlaka, na Yeye. Roho yule yule aliyekuwa ndani Yake, yuko ndani yenu. Vema.

¹⁷¹ Ishirini na tano, ishirini na sita, ishirini na saba, ishirini na nane, ishirini na tisa, thelathini, hebu hao waje. Tunawaita hivyo ili tusiwe na msongamano, mwajua, kutembea huku na huku sana. Vema, thelathini, thelathini na moja, thelathini na mbili, thelathini na tatu, thelathini na nne, thelathini na tano, thelathini na sita, thelathini na saba, thelathini na nane, thelathini na tisa, arobaini. Hiyo ni sawa, songeeni tu moja kwa moja pale chini nao watawaweka mstarini. Endapo huwezi kutembea, mbona, mjulishe mtu fulani, watakubeba.

¹⁷² Sasa, ni wangapi wasio na kadi ya maombi, inua mkono wako, useme, “Ninataka Mungu aniponye alasiri ya leo.” Sijali wewe ni nani, unakotoka, chochote kile, sema tu, “Nataka Mungu aniponye. Ninaamini.”

¹⁷³ Vema, arobaini hadi hamsini sasa, hebu waje. Kila mtu aliye na kadi ya maombi, simama na uje hapa sasa, wewe uliye na kadi yako ya maombi. Tutangojea tu dakika chache na kuanza moja kwa moja mstarini, kuwaomba wagonjwa.

¹⁷⁴ Sasa, tunapaswa kuwa tumemaliza katika dakika kumi ama kumi na tano zijazo, kwa hiyo nivumilieni kidogo, na mwombe kwa yote yaliyo ndani yenu. Sasa ninawatakeni mwangalie huku, kila mmoja wenu sasa. Sasa kumbukeni. . .

¹⁷⁵ Kuna wageni wowote hapa ambao hawajawahi kuwa katika mmoja wa hii mikutano hapo awali? Wapo kiasi, hebu angalieni. Tuna furaha sana kuwa nanyi. Tukitumaini kwamba m—mtaendelea katika ibada ya aina hii, hiyo ni kusema, ambapo Roho Mtakatifu... Endapo wewe si m—mfuasi wa kanisa ambalo ni la Injili yote, na kwa asili, tungekuomba, endapo unapenda aina ya ibada ambapo Roho Mtakatifu anaingia na kutenda kazi. Waangalie wahudumu hawa hapa, wa—wanaishi

kote humu nchini hapa, nao wataninii. . . (Asante, dada.) Wata—watafurahi kuwa nawe kanisani mwao.

¹⁷⁶ Sasa nataka kusema hili, kwamba kila mtu ambaye ameongoka juma hili, kila mtu ambaye ameongoka hapa juma hili, sasa, angalia kundi hili la wahudumu, wa—wanatetea jambo lile lile ninalolitetea. Hatuna tofauti hata kidogo. Sisi ni sawa kabisa. Tunaamini katika Injili yote, ubatizo wa Roho Mtakatifu, mambo haya yote. Wahudumu hawa wote hapa, sisi sote ni sawa kabisa. Nasi tunawatakeni mjiunge na kanisa lao kusudi mpate kuendelea. Sasa wao ni. . . Msamaria mwema amepitia hapa, akatia kidonda mafuta. Lakini amekuchukua sasa, naye anakutaka uende kwenye moja ya mikahawa hapa, ulio karibu nawe. Tayari amemlipa mchungaji kukuhudumia, kwa hiyo yeye amelipwa; alimpokea Roho Mtakatifu, akapata baraka za Mungu, na afya, na ufunuo, anaweza tu kuilisha nafsi yako! Kwa hiyo njoni sasa mkajiunge na moja ya haya makanisa, nalo lita—litakuwa ndilo jambo zuri kuliko yote unaloweza kufanya kuidumisha roho yako ikiwa imeshiba na kusonga mbele. Mungu awe pamoja nanyi.

¹⁷⁷ Sasa, hatudai kuwa chochote zaidi ya ndugu yenu. Sasa, kama Unyakuo ukija leo hii, na Mungu angewapeleka nyumbani wale wanaostahili kwanza, mimi ningekuwa wa mwisho kuondoka humu jukwaani. Hiyo ni kweli. Nilizaliwa nje ya wakati. Mimi. . . Wakati ninyi, wengi wenu wahudumu wa Kipentekoste hapa, wenye umri mkubwa kuliko wangu, miaka mingi iliyopita mlikuwa hapa nje mtaani, mkihubiri, wakati mateso yalipokuwa makali, mlikuwa mkiitengeneza njia ninayokimbilia sasa. Mlikuwa mkiwaambia watu ya kwamba mambo haya yangetukia. Iliwabidi kufyeka kila namna ya vichaka na kadhalika, juu ya kila namna ya lundo la mawe. Mnaona? Mimi ni mtoto mchanga tu. Nanyi ndinyi, ninyi ndio ndugu ambao—ambao mmeuleta huu. Ninyi ndinyi ndugu na dada ambao mmefanya mambo haya. Mliunena tu kwa watu, mkawaambia kwamba ungekuja. Mliweka msingi. Mmoja ni. . . huweka msingi, huyo mwingine ni seremala, mmoja ni fundi bomba, mwingine ni fundi umeme. Nyumba ya Mungu inajengwa. Mnaona? Na sasa wakati tukiendelea, kila mtu ana mahali pake. Na sasa sisi—sisi tunataka watu wawaheshimu na kuwapenda ndugu zetu na makanisa haya. Na kuuacha Ufalme wa Mungu ukue na kuongezeka kila mara, ndilo ombi letu.

¹⁷⁸ Sasa, siwezi kuponya. Uponyaji tayari umenunuliwa na Roho Mtakatifu. Ni wangapi wanaojua hilo? Kristo alifanya hivyo pale Kalvari. Jambo pekee, kwamba labda watu hawa hapa, wao ni wahudumu, wangeweza kulichukua Neno la Mungu. Nisingeninii. . . Nisingethubutu kusimama mbele yao pamoja na Neno la Mungu, na chochote kinyume; kwa sababu, wameitwa, hiyo ni ofisi yao, wanahubiri, wanajua wanachozungumzia. Kwa hiyo mimi husikiliza tu wasemayo, na

kusema “amina” na kuendelea, maana wao ni—wao ni watu wa Mungu. Ninawafuata, nami ninakuta kwamba wako katika Biblia, na wanasema Kweli.

¹⁷⁹ Vema, sasa, mimi sana sana si mhubiri. Lakini karama yangu ni karama ya kuona. Hiyo ni... Yesu alikuwa muhubiri. Yeye pia alikuwa ni mwonaji. Na kwa upande wangu, kwa kuwa sina elimu ya kutosha kuhubiri, bali ninayo karama ya kuona mambo kimbele, kutabiri na kusema kimbele.

¹⁸⁰ Kwa kuwa, katika Biblia, ilisema, “Walitumwa mitume, manabii, wainjilisti, walimu, wachungaji, hawa wote kwa ajili ya kukamilishwa kwa Kanisa.” Mungu aliwaweka Kanisani. Sasa, kuna karama tisa za kiroho, ambazo tunaweza kuzishikilia, na kadhalika, na kuomba kwa bidii kwa ajili ya karama zilizo bora zaidi, na kutabiri namna hiyo. Lakini hizi zingine ni karama zilizokusudiwa tangu zamani na Mungu, Mungu huziweka Kanisani.

¹⁸¹ Kwa wakati ambao unakuja, Yeye... Yohana Mbatizaji, alikuwa ni mtangulizi maalum wa wakati huo. Mungu alimkusudia tu tangu zamani kuifanya kazi hiyo. Mnaamini hilo? Hakika, alimkusudia. Yesu alisema, “Mlienda kumwona nabii?” Kasema, “Zaidi ya nabii.” Mnaona? Yohana hakujua hilo, bali Yesu alijua. Mnaona?

¹⁸² Naye Yeremia, kabla hajazaliwa, Mungu alisema, “Nilikujua, nikakutakasa, na kukuchagua nabii kwa mataifa.” Hiyo ni kweli, sivyo?

¹⁸³ Sasa, wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, alisema, wakati alipokaribia kuondoka, alisema, “Kitambo kidogo, na ulimwengu...” Usisahau hili, rafiki Mkristo. “Kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena; hata hivyo ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.” Je, alisema hivyo? Angekuwa pamoja nasi hata ukamilifu wa dahari. Biblia ilisema ya kwamba “Yeye ni yule yule jana, leo na hata milele.” Hilo linamaanisha, “yeye yule katika kanuni, yeye yule katika nguvu.” Jambo pekee lililo tofauti katika Yesu leo hii duniani, kuliko vile alivyokuwa wakati huo, leo hii Yeye yuko hapa katika mfano wa Roho Mtakatifu. Mwili Wake wa kawaida umewekwa mkono wa kuume wa Mungu Mbinguni. Siku moja Yeye atakuja, nao walio katika Kristo watafufuka waende pamoja Naye. Mnaona? Hilo ndilo tunalotazamia, siku hiyo. Lakini Roho Wake, pamoja na nguvu Zake zote na dhihirisho, ametolewa kwa Mwili wa waaminio kote ulimwenguni.

¹⁸⁴ Sasa, Malaika huyu wa Bwana: kama hatafanya na kutenda kazi zile zile ambazo Yesu alifanya, basi siye Roho aliyekuwa juu ya Yesu, bali kama *akitenda* kazi zile zile alizofanya Yesu! Kwa sababu Yeye alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo, yeye naye atazifanya.”

¹⁸⁵ Mnajua Biblia inasema, mlango ule ule, Yohana 14, “Kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya; hata *nyingi zaidi* ya hizi atazifanya, kwa kuwa ninaenda kwa Baba Yangu.” Ninajua King James inaliweka “kubwa zaidi.” Haingeweza kuwa kubwa zaidi; ile ya asili inasema “nyingi zaidi.” Maana, Yeye alisimamisha maumbile, aliwafufua wafu, vema, kila kitu tu. Usingeweza kufanya kubwa zaidi ya alizofanya Yeye. Lakini Kanisa litafanya nyingi zaidi yazo, kwa kuwa, wakati tukiwa na mkutano hapa, wanafanya mkutano huko Afrika, wanayo huko Brazil, wako kote ulimwenguni, mnaona, hakika zingeweza kuwa *nyingi zaidi*. Mungu alidhihirishwa katika Mtu mmoja wakati huo, Mwanawe Yesu; sasa Yeye amedhihirishwa katika Kanisa Lake, kote ulimwenguni. Lakini Roho yule yule akifanya kazi zile zile! Siku moja . . .

¹⁸⁶ Kweni ninyi msio na kadi ya maombi. Sasa, kuna kadi moja zaidi ya maombi kwenye—kwenye kusanyiko? Ikiwa ipo, inakupasa kuingia mstarini. Ninyi msio na kadi za maombi, kulikuwako na mwanamke . . .

¹⁸⁷ Hebu tuseme—hebu tuseme hivi, halisemi hivi, bali mwanamke wakati mmoja alikuwa na kutokwa na damu, naye hakujua jinsi atakavyomfikia Yesu. Lakini akasema, “Kama ninaweza kugusa upindo wa vazi Lake, ninamwamini, nitaponywa.” Ni wangapi waliopata kuisoma hadithi hiyo? Mbona, hakika, tuliisoma.

¹⁸⁸ Basi, sasa, akapenya kisiri kwenye huo umati, akapenya kupitia wakosoaji wote, naye akaligusa vazi Lake. Sasa, vazi la Kipalestina lilining’inia kwa kupwaya, pia walikuwa na vazi la ndani. Sasa, Yeye hakuhisi hilo kimwili, bali alisema, “Ni nani aliyenigusa?” wakati alipomgusa kisha akarudi kwenye kusanyiko. “Ni nani aliyenigusa?”

¹⁸⁹ Na, mbona, Petro akamkemea, akasema, “Bwana, kwa nini kusema jambo kama hilo? Mbona, kila mtu anakugusa, na Wewe wasema, ‘Ni nani aliyenigusa?’” Akamkemea, Biblia ilisema.

¹⁹⁰ Akasema, “Lakini naona kwamba nimekuwa dhaifu, nguvu zimenitoka.” Ndipo akaangalia kote juu ya hilo kusanyiko mpaka akampata maskini mwanamke huyo. Naye akamwambia, “Imani yako imekuokoa.” Alikuwa akitokwa na damu. Mnakumbuka hilo? Sasa, ni wangapi . . .

¹⁹¹ Angalieni, hawa makasisi hapa, ninyi nyote ni wachungaji. Ndugu wachungaji, Biblia ilisema kwamba “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Je, hiyo ni kweli? Nayoy Biblia inasema ya kwamba “Yeye ni Kuhani Mkuu, anayeketi mkono wa kuume wa Mungu sasa, akituombea tunapokiri.” Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Hiyo ni kweli? Mnaona hilo? Kuhani Mkuu. Sasa, iwapo Yeye ni yeye yule jana, leo na hata milele, mguso wa namna ile ile ungesababisha matokeo yale yale. Hiyo ni kweli?

¹⁹² Sasa wewe mwangalie Yeye. Ungewezaje kumgusa? Kwa imani yako. Mkaribie useme, “Bwana Yesu, nina haja muhimu sana.”

¹⁹³ Sikiliza. Omba hili. Usijiombe mwenyewe; mwombee mtu mwingine. Hebu tulichukue hivyo. Sio kama wewe mwenyewe; mwombee mtu mwingine. Roho Mtakatifu na ashughulikie hilo. Mwombee tu mtu mwingine. Baadhi ya wapendwa wenu, ama mtu fulani unayejua yuko mahali fulani, ama kitu kama hicho, mwombee huyo. Unaona, upate kujua... usininii... Si lazima wawe hapa. Mungu husikia maombi. Yeye anajua kile unachoombea.

¹⁹⁴ Ni wangapi humu jengoni tusiofahamiana, ambao sijui chochote juu yenu? Inua mkono wako. Asanteni. Nadhani, kila mtu. Kwenye mstari huu wa maombi, kila mmoja wenu anajua, unajua hatufahamiani, inua mkono wako. Sikujui.

¹⁹⁵ Sasa, mnatambua, kama mguso mmoja kutoka kwa maskini mwanamke mmoja ulimfanya Yesu Kristo Mwana wa Mungu dhaifu, nguvu zilimtoka (*nguvu* ni “uweza”), mstari huo ungenifanyaje mimi, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema? Mnaona, hiyo hapo fasiri yenu, “*Nyingi zaidi* ya hizi mtazifanya.” Mnaona? Haya basi. Sasa, kama ningechukua nusu ya mstari ule wa maombi, kwenye upambanuzi, labda wangenibeba wanitoe nje. Linanidhoofisha tu. Kuna jambo fulani kulihusu. Siwezi kufanya huo wote. Lakini ninaweza kumwombea kila mmoja. Hivyo ndivyo mnavyotaka, kwa vyovyote vile, sivyo jamani?

¹⁹⁶ Kuwawekea mikono. Sasa, Yesu, Yeye hakusema, “Wekea mikono na uombe.” Alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa.” Kamwe hakusema “waombeeni”; “wawekeeni mikono” tu. Utaratibu wa kuomba ni, “Waite wazee wa kanisa, wawapake mafuta na kuwaombea,” hiyo ni kwa ajili ya kanisa. Lakini karama ya kiinjalisti ya uponyaji ni “kuwawekea wagonjwa mikono” tu. Tunajua hilo. Sio “waombeeni”; “Wawekeeni mikono, ishara hizi zitafuata!” Sasa, lakini ili kwamba...

¹⁹⁷ Hebu tuone, ni nani... Ndugu Borders, nani? Vema. Ili kwamba tu Roho Mtakatifu aweze kuanza, kutenda kazi miongoni mwetu.

¹⁹⁸ Sasa, angalieni, sitaki mtu yeyote kusogea huku na huku. Tafadhali, sasa, kila mahali, iweni watulivu sana, iweni na kicho. Sasa, ninamaanisha, wakati Roho Mtakatifu anapofanya jambo lolote, ukitaka kumsifu, hilo ni sawa, unapaswa kufanya hivyo. Lakini usitembee huku na huku. Keti kimya. Maana, kila mmoja wenu ni roho. Ndipo basi upako wa Roho Mtakatifu unakuja na, tuseme, mtu fulani huko nyuma kule akisema, “Sijui kama hilo ni kweli,” ninahisi hilo papa hapa. Mtu fulani huko nyuma kabisa akisema, “Aisee, John, unamjua *Fulani-wa-fulani* na *Fulani-wa-fulani*? Nilikuwa *ninii*.” Mnaona, hilo linasumbua.

199 Mnaona, kwa sababu, kama yule Roho mkuu wa Uzima wa Milele yuko pamoja nasi, Naye amenipaka mafuta kwa ajili ya jambo fulani, basi nitalihisi kama pigo la moyo. Mnaona, ninyi... Hivyo ndivyo ni—ninavyoliona. Mnaona, unamgusa Yeye. Basi kupitia hapo, unapomwomba Yeye, kibali chako na imani yako inamgusa; ndipo Yeye ananinii tu... Ninajisalimisha tu, halafu Yeye ananena, na kuanza kuniambia. Basi nyinyi iweni hakimu kama ni kweli ama si kweli.

200 Sasa endapo atafanya hili kwa mara ya mwisho, sasa tunaondoka, tunajiandaa, huu mkutano uko karibu kumalizika katika dakika zingine chache, ni wangapi watakaosema, “Nitalikubali kwa moyo wangu wote, na kuamini kwa chochote ninachohitaji”? Mungu awabariki sasa.

201 Baba wa Mbinguni, katika mikono Yako naliweka kusanyiko hili. Nachukua kila roho hapa chini ya mamlaka yangu, kwa ajili ya heshima na utukufu wa Yesu Kristo. Ninaomba katika Jina Lake. Amina.

202 Sasa, huyu mama hapa, ninaamini (ndio kwanza ainue mkono wake) kwamba alikuwa mgeni kabisa kwangu. Simjui. Labda mara yetu ya kwanza tuliopata kuwa karibu hivi pamoja, isipokuwa iwe tulipitana mtaani mahali fulani. Lakini Mungu anatumia sote wawili. Sasa iwapo...

203 Sasa angalieni, enyi marafiki. Hii hapa picha leo hii ya Yohana Mt. 4, mwanamke na mwanamume wakikutana kwa mara yao ya kwanza; Yesu na mwanamke wa Samaria. Sasa, mimi si Yesu, wala yeye si huyo mwanamke wa Samaria, bali ni wakati mwingine. Roho Wake yeye yule yuko hapa. Huyu mwanamke anayesimama hapa, huenda akawa ni mkosoaji, huenda akawa ni Mkristo, huenda akawa ni mwigaji, huenda anahitaji pesa, huenda amesimama kwa ajili ya mtu mwingine. Sijui mimi. Nisingeweza kuwaambia. Lakini Mungu anajua. Sasa iwapo Yeye atasimama na kuniambia, na kumwacha awe hakimu, iwapo Yeye ataniambia, kikamilifu, jambo fulani kumhusu! Kama mimi...kuna jambo lolote kumhusu, nisingejua. Lakini kama Yeye angeniambia jambo fulani kumhusu yeye, acheni awe ndiye hakimu.

204 Halafu, vema, kama ni kweli, mnajua itabidi itoke kwenye nguvu za namna fulani. Hiyo ni kweli? Baadhi...Vema, basi ungeziainishaje hizo Nguvu? Ni kuhubiriwa kwa Injili, kumtukuza Yesu Kristo, kuwaita wenye dhambi madhabahuni, kuwaponya wagonjwa na wanaoteseka, ni Roho wa aina gani, huyo Roho angekuwa akizaa matunda ya aina gani? Matunda ya aina ile ile ambayo Yesu Kristo alizaa, akiwa na Roho wa Mungu juu Yake. Hiyo ni kweli? Ingekuwa ni Roho wa Kikristo. Hakika, ingekuwa ni juu yako kujichagulia, ni yupi.

205 Lakini ingekuwa ni Mungu kwako, sivyo? [Huyo mwanamke anasema, “Naam, ingekuwa hivyo.”—Mh.] Naam. Hakika, yeye

ni Mkristo.

²⁰⁶ Sasa, nilijua je alikuwa ni Mkristo? Maana ninaihisi Roho yake, mnaona, sasa hivi, kama tu pigo la moyo likiingia, kama kufanya, *whiu, whiu, whiu*. Nami ninajua Roho wa Mungu aliye juu yangu, anayenipaka mafuta sasa, anatambua ya kwamba huyo ni dada yangu. Nami sijawahi kumwona, hata hivyo ninajua kwamba ndivyo alivyo. Mnaona, ni kama tu kitu kikiingia namna *hii*. Ni kuambatana. Roho yake inaungana pamoja na Roho aliyenipaka mafuta.

²⁰⁷ Ni wangapi wameiona ile picha ya Malaika wa Bwana? Wanazo, loo, wanazo hapa kila mahali, ziko kote ulimwenguni. Kumbukeni, nawaambia jambo hili. Malaika huyo wa Bwana mnayemwona kwenye hiyo picha, ile Nguzo ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli, iliyofanyika mwili na kukaa miongoni mwetu, iliyotoka kwa Mungu na ikaenda kwa Mungu, inarudi katika siku za mwisho kufanya kazi Zake, kuumaliza Ufalme, iko papa hapa ndani ya inchi sita za mahali ninaposimama. Sasa kumbukeni hilo. Ni changamoto jinsi gani! Lakini ninamwamini Yeye. Yeye anajua. Ninajua ya kwamba Yeye hashindwi kamwe.

Sasa kama Bwana atanifunulia jambo fulani kukuhusu, dada.

²⁰⁸ Na kwenu mlio kwenye mstari wa maombi, sasa ninyi iweni tayari tu, maana sitaki kusimama kufanya upambanuzi juu ya wote, maana hiyo . . . nisingeweza kufanya hivyo. Lakini ninyi iweni tu tayari, iweni mkiamini.

²⁰⁹ Sasa, kama ningeweza kuwasaidia, wala nisiwasaidie, basi ningekuwa mwovu, sipaswi kuwa nimesimama hapa kwenye mimbara hii; mtu wa aina hiyo, la hasha. Lakini nimekuwa nikihubiri kwa nguvu. Nami ninangojea tu kwa dakika moja, nipate kufanya mazungumzo nawe.

²¹⁰ Kama vile tu Bwana wetu alivyomfanyia yule mwanamke kisimani, Yeye alisema, “Nipe maji ninywe.” Unaona? Alikuwa akifanya nini? Kuishika roho yake, aone kile—kile kilichokuwa shida. Basi alipoipata shida yake, alimwambia shida yake ilikuwa ni nini. Unakumbuka ilikuwa ipi? Alikuwa na waume watano; na sita, ndivyo ilivyokuwa, maana alikuwa na watano na yule aliyekuwa akiishi naye wakati huo alifanya waume sita.

²¹¹ Basi—basi alipomwambia shida yake ilikuwa nini, mbona, alisema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii.”

²¹² Mnaona, wa—wa—wale Mafarisayo walikuwa tu wamesema “Yeye alikuwa ni mpiga ramli, ibilisi.” Yeye akawaambia ya kwamba wangesamehewa hilo wakati huo. Lakini Roho Mtakatifu akija, kufanya hivyo, kamwe kusingesamehewa, kunena dhidi Yake.

213 Kwa hiyo, lakini yeye akasema, “Naona kwamba Wewe ni nabii. Nasi tunajua (sisi Wasamaria, tunajua Neno), tunajua ajapo Masihi, Yule aitwaye Kristo, atatwambia mambo haya yote.” Mnaona, yeye alijua ya kwamba hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi.

Naye akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

214 Basi akaacha mtungi wa maji, akakimbia mjini, na kusema, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?”

215 Sasa, iwapo hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi wakati huo, ingekuwa ndiyo ishara ya Masihi sasa, ikiwa Masihi ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Kama Roho huyu ambaye. . .

216 Unatambua, ya kwamba jambo fulani linaendelea, sivyo? Sasa hebu kusanyiko lijue. Hisia tamu kweli, nyenyekevu imekuwako sasa hivi, iko juu yako. Sivyo? [Dada huyo anasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Inua mkono wako. Tamu sana, nyenyekevu. Ninaangalia ile Nuru kati yangu na huyu mwanamke. Sasa inaondoka.

217 Huyu mwanamke anaugua TB. Naye ndio kwanza atoke kwenye hospitali ya kifua kikuu. Hiyo ni kweli. Kunaye mtu mwingine. Ni mvulana huyu hapa. Hebu kidogo. Roho yuyo huyo juu yake. Vema, huyo ni mjukuu wako. Hiyo ni kweli. Yuna ugonjwa wa uwazi wa pua. Pia ana tishu yenye kovu kwenye pafu lake. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, sivyo? [Dada huyo anasema, “Hiyo ni kweli. Ni kweli. Madaktari walisema alikuwa nao.”—Mh.] Hakika. Vema. Bibi Harris, hilo ndilo jina lako. [“Hilo ndilo jina langu.”] Wewe pamoja na mjukuu wako nendeni nyumbani, shida zenu zimekwisha. Yesu Kristo anawaponya. . . ? . . .

218 Mnamwamini Bwana Yesu sasa? Mnaona, hiyo ni Biblia, huyo ni Roho wa Mungu akifanya yale yale jana, leo, na hata milele. Sasa unaamini kwa moyo wako wote? Hilo linapaswa kulitatua.

219 Sasa kama sitasema neno moja, niweke tu mikono yangu juu yako wakati Upako ukiwa hapa, ungeamini? Nenda basi, ukaponywe, katika Jina la Yesu Kristo.

220 Njoo, dada. Unataka kuponywa shida yako ya tumbo? Nenda tu, ukimshukuru Mungu, na kusema, “Imekwisha,” amini kwa moyo wako wote.

221 Kama nikiweka mikono yangu juu yako, unaamini Mungu atakuponya? Katika Jina la Yesu, ponywa. Huo ndio msimamo wa kuingia. Yeye aliponywa. Hiyo ni kweli. Huo ndio msimamo. Sasa, kumbukeni, Roho Mtakatifu yuko hapa.

222 Huyu hapa anakuja maskini mvulana mdogo anayependeza. Wewe ni mdogo sana, kipenzi, ni vigumu, kuwa na imani. Lakini angalia hapa kwa dakika moja, mwangalie Ndugu Branham.

Vema. Tatizo lako la moyo limekwisha sasa. Unaweza kwenda nyumbani na uwe mzima. Amina. Yesu anakupa afya.

223 Hebu tuseme, “Mshukuru Bwana,” kwa ajili ya mvulana huyo mdogo.

224 Umekuwa na wasiwasi sana, sivyo? Utakuacha sasa. Nenda tu moja kwa moja nyumbani, ukisema, “Asante, Bwana,” na ukaponywe.

225 Njoo. Vema, maskini kisukari hicho, laiti tungaliweza kukiondoa! Unaamini kwa moyo wako wote? Katika Jina la Yesu, jalia kimwache huyu mwanamke wala kisimsumbue tena. Amina.

226 Njoo sasa. Mama huyu alikuwa na kitu kile kile, kisukari, pia. Amini kwa moyo wako wote sasa unapopitia hapa, na ukaponywe, katika Jina la Bwana Yesu.

Mnaamini, kila mtu sasa? Mwaminini Mungu!

227 Njoo, dada yangu. Katika Jina la Yesu Kristo, uponywe. Kuwa na imani, usitie shaka.

228 Njoo, ndugu mpendwa. Kweli ninaamini uliponywa wakati ulipokuwa umeketi chini pale, kwa hiyo unaweza tu kuendelea mbele! . . . ? . . . Mungu akubariki sasa. Vema.

229 Njoo, dada mpendwa. Mwamini Mungu! Jambo ndilo hilo. Jambo ndilo hilo. Katika Jina la Yesu Kristo, ponywa. Amina. Mungu akubariki, dada. Endelea moja kwa moja, ukishangilia na kuamini. Loo, huo ndio msimamo wa kuingia.

230 Sasa iweni na kicho kabisa, kila mmoja kaeni vitini mwenu sasa. Iweni na kicho kabisa, Roho Mtakatifu yuko hapa. Kwa sababu tu hawazungumzii sana; wakati mwingine anasema tu mambo. Ninajaribu tu kusema. . . Na kama nikimwona akitokea upesi sana, ninalisema halafu basi ninaendelea mbele. Mnaona? Wakati mwingine ninaweza kutoka upesi kwake tena kwa dakika chache, kisha ninaendelea. Lakini Roho Mtakatifu yuko hapa, Yeye angali anajua mambo yote.

231 Unaamini hilo, mama? Njoo karibu nami. Nina hakika, wewe ukiwa ni Hispania, nami Mwairishi, hatufahamiani. [Dada huyo anasema, “La.”—Mh.] Hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana. Unaamini Yesu Kristo, Huyu ambaye ninanena habari Zake, ndiye Mwana wa kweli wa Mungu? Unaamini mimi ninamwakilisha vizuri? Unaamini Yeye alinituma kukusaidia? [“Naam.”] Kama nikikwambia shida yako ni ipi, utamwamini? Shida yako iko mgongoni mwako. Una tatizo la mgongo. Pia, mume wako ana tatizo la mgongo. Ana tatizo la mguu wake. Una msichana aliye na tatizo la shingo. Lilisababishwa na ajali ya motokaa. Hiyo ni kweli. Nenda nyumbani, nyote mtakuwa sawa.

232 Kuwa na imani. Usitie shaka. Sasa hilo hudhoofisha na kufanya jambo fulani. Iweni na imani sasa, aminini.

Katika Jina la Yesu, ninamwombea huyu mwanamke. Amina.

²³³ Njoo sasa. Njoo, bwana. Usitie shaka sasa. Umekuwa na wasiwasi sana na kushtuka, na kukufanya uwe na donda la pepsini tumboni mwako, na linakuuma. Lakini nenda nyumbani sasa, utapata afya na uwe mzima. Mungu akubariki. Kuwa na imani sasa. Amini kwa moyo wako wote.

²³⁴ Vema, tunaweza kuona tatizo la mtoto mchanga, amevaa magango yake hapa. Utaamini kwa niaba yake, dada, sasa? [Dada huyo anasema, “Ndiyo, ninaamini.”—Mh.], Kwamba Mungu atamjalia maskini msichana huyo kuishi, na kukua awe msichana mzuri bila magango haya?

²³⁵ Baba mpendwa wa Mbinguni, kama ningaliweza kumponya mtoto huyu na kumtoa magango haya, ningemponya. Lakini ninaweka mkono wangu juu ya mtoto huyu mpendwa, ambaye hana njia ya kuwa na imani kwa ajili yake mwenyewe. Ninalaani hali hii ya ulemavu. Katika Jina la Yesu Kristo, mtoto huyu na atembea na kuishi.

Hakika tu kama ninavyosimama hapa. [Dada huyo anasema, “Amepona.”—Mh.] Hakika. Naam. Unaamini hilo, sivyo? [“Ninaamini.”] Ni wangapi wanaoamini hilo? Yeye ataenda, na mtoto huyo mchanga atatolewa hayo magango, naye atatembea. Vema, iweni na imani.

²³⁶ Tumbo lililokufa ganzi. Na, loo, jamani! Unaamini? Basi nenda moja kwa moja, na ule na uwe na wakati mzuri, basi imani yako imekuponya.

Iweni na imani sasa, kila mtu, mwaminini Mungu! Njoo, dada mpendwa. Unaamini kwa moyo wako wote?

²³⁷ Ee Bwana, ninaomba ya kwamba Wewe utamponya. Hana budi kupata nguvu Zako za uponyaji, la sivyo atakufa. Nami ninaomba ya kwamba Wewe utamponya. Lijalie. Lijalie.

²³⁸ Vema, dada. Hebu nikuonyeshe jambo fulani. Kuna watu wengi sana huko nje kwenye kusanyiko, wanaoteseka na jambo lile lile linalokusumbua. Mnaona, hebu nikuonyeshe jambo fulani. Una moyo wenye wasiwasi. Hebu nikuonyeshe huko nje. Wote wanaosumbuliwa na wasiwasi (inueni mikono yenu) na moyo, inueni mikono yenu. Waangalie, unaona. Ningewezaje kuita kila mmoja wao? Mnaona? Nisingeweza kufanya hivyo. Lakini ninaweza tu kuhisi maafikiano hayo makubwa; adui akijaribu kukushikilia, na akilia huko nje apate rehema. Atapoteza mshiko wake kila mahali. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, unaamini atapoteza, kwamba aliupoteza juu yako sasa hivi? [Dada huyo anasema, “Naam.”—Mh.] Unajisikia tofauti, sivyo? Uliponywa wakati huo tu. Nenda zako, ukishangilia, useme, “Asante.”

239 Njoo, msichana, amini kwa moyo wako wote na uponywe. Katika Jina la Yesu, dada yetu na aponywe.

240 Mungu, ambariki mvulana huyu mdogo usiku wa leo. Loo, jamani! Unaamini Yesu atakuponya? Vema. Katika Jina la Yesu! Mungu akubariki.

241 Vema. Njoo sasa, na uamini, ndugu. Njoo, ndugu yangu, bawabu. Njoo, wewe, pata baraka za Bwana. Ninaweka mikono yangu juu ya ndugu yangu, katika Jina la Yesu. Jalia aponywe. Lijalie.

242 Kila mtu anaamini? Iweni na imani. Msiwe na shaka. Aminini tu sasa. Kwa sababu tu hatutulii kwa kila mtu, hilo halimaanishi...Kusema tu...Ninaliona, bali sitaki hilo ono lininii...Ni kitu fulani kinachounganisha ndani yako unapozungumza na watu. Mnajua ninachomaanisha? Kinaunganisha, halafu wewe...Jambo ndilo hilo, unaona, wewe...Kinakudhoofisha.

243 Hebu kidogo, jambo fulani lilitukia kwenye kusanyiko hili. Kama utaamini, kamwe haitakubidi kufanyiwa upasuaji huo wa kibofu. Uliugusa upindo wa vazi Lake, dada. Yeye aligusa nini? Niambieni alichogusa. Haiwezekani kwake kunigusa kutoka pale. Lakini alifanya ninii tu...Sasa hebu niwaambieni jambo fulani. Alikuwa ameketi hapo hapo wakati huo, akiomba, "Mungu, jalia aniite." Iwapo hiyo ni kweli, kama hilo ndilo ombi lako...Hilo hapo, unaona. Hiyo ni kweli kabisa. Wewe fanya vile vile, uone kama sivyo ilivyo. Fanya tu vivyo hivyo. Vema.

244 Hatufahamiani. Sikujui wewe, wala wewe hunijui. Mungu anatujua sote wawili. Wakati Upako ukiwa hapa, tutaona tu tatizo ni lipi. Jambo la kwanza, unasumbuliwa na macho yako, kichwa chako. Una fundo kwenye mkono wako wa kushoto na kwenye kifundo cha mkono wako. Hiyo ni kweli. Unaamini? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Umetoka mahali panapoitwa Sunnyvale. Um-hum. Bibi White. Nenda nyumbani, ukishangilia, na upate afya. Vema.

245 Mwaminini Mungu, aminini tu sasa, kila mmoja. Njoni sasa na mwe...Mnaamini? Kila mtu anaomba? Loo, kaeni tu mbele za Mungu, mkiomba!

Njoo, ndugu. Katika Jina la Yesu, ponywa.

246 Njoo, dada mpendwa. Njoo, ukiamini kwa yote yaliyo ndani yako. Ee Bwana, katika Jina la Yesu, mponye dada yangu. Amina.

247 Njoo, dada mpendwa, amini tu yale Mungu anayofanya, Uwepo Wake. Unapitia chini ya msalaba sasa. Katika Jina la Yesu, naomba aponywe.

248 Njoo, dada, ukipitia chini ya msalaba, ukiamini kwa moyo wako wote. Ugonjwa wa mgongo utaondoka, nawe unaweza kwenda nyumbani uwe mzima. Vema. Katika Jina la Yesu Kristo!

249 Njoo, dada mpendwa. Ee Bwana, ninaomba, wakati akipita, ya kwamba Wewe utamponya. Amina.

250 Njoo, dada. Amini sasa. Wahudumu, ombeni. Kila mtu aombe. Njoo. Katika Jina la Yesu, jalia aponywe. Amina.

251 Njoo sasa, amini kwa moyo wako wote. Maskini dada, yuko mahututi sana. Unaamini Mungu anajua shida yako? Unaamini anaweza kuniambia? Basi tatizo hilo la kike limekoma. Nenda zako nyumbani upate afya.

252 Njoo, ukiamini. Vema, dada mpendwa, njoo huku. Unaamini kwa moyo wako wote? Unafikiri uliponywa muda mfupi uliopita wakati tulipowaomba wale waliokuwa na ugonjwa wa moyo huko nje? Unaamini? Endelea moja kwa moja, uponywe, na uamini kwa moyo wako wote.

253 Hebu tuseme, “Bwana asifiwe,” kila mtu. Mwaminini Mungu.

254 Njoo, ndugu yangu. Katika Jina la Bwana Yesu, naomba aponywe. Amina.

255 Hilo si ni zuri sana? Yeye si ni wa ajabu sana? Si ajabu aliitwa “Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenyezi, Baba wa Milele”!

256 Waombeeni wapendwa wenu. Ombeni tu (sio kwa ajili yenu wenyewe) kwa ajili ya wapendwa wenu kwa dakika moja tu. Mwombee mtu fulani.

257 Mama, unaamini? Unaamini Mungu anaweza kuniambia unasimama hapa kwa sababu gani? Ninaona una ninii. . . Loo, wewe ni mmoja wa wafanyakazi? Sikujui wewe. Na—nadhani sijapata kukuona si zaidi ya huko kwenye kusanyiko. Hiyo ni kweli? Kusudi hili kusanyiko lipate kujua. Hiyo ni kweli. Unaamini Kristo anaweza kunifunulia shida yako ni gani? [Dada huyo anasema, “Amina.”—Mh.] Na kama akifanya hivyo, basi. . . Naam, kwa kuwa amevaa kibandiko hicho, mtu fulani huenda akawa humu ndani na kusema, “Vema, hakika, yeye ni mfanyakazi, alimfahamu.” Sijawahi kukutana nawe maishani mwangu, sijui chochote. Lakini kama nikikwambia mahali shida yako ilipo, na jambo fulani, unajua lazima iwe ni kitu fulani mbali na mimi kufanya hivyo. Hiyo ni kweli? [“Hiyo ni kweli.”] Huko hapa kwa ajili yako mwenyewe. Uko hapa kwa ajili ya mwanao. Hiyo ni kweli. Naye ana shida na misuli yake. Kidogo ni kuoza kwa misuli. Ilimfanya kushikwa na ugonjwa fulani, macho yake yakawa makengeza, na kadhalika, wasiwasi kweli. Jina Lake ni Donald. Nenda zako nyumbani, na uamini, uache apate afya. Chukua lesa hiyo. . . ? . . .

258 Mwaminini Mungu. Msiwe na shaka. Naomba uje, dada. Njoo, ukiamini. Sasa na tuombe, kila mmoja awe katika maombi. Njoo, dada. Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, jalia dada yangu aponywe.

²⁵⁹ Njoo sasa, dada mpendwa. Hiyo ni kweli, njoo huku. Ee Bwana, wakati akipitia chini ya msalaba wa Kristo, jalia Damu iuguse mwili wake.

²⁶⁰ Njoo, dada yangu mpendwa, amini kwa ajili ya huyu mtoto mchanga. Na, Bwana, wakati wakipitia chini ya msalaba, ninaweka mikono yangu juu yao na kuombea uponyaji wao, katika Jina la Yesu.

²⁶¹ Njoo, ndugu yangu, pitia chini ya msalaba, ukiamini kwa moyo wako wote. Uliyoomba yatakuwa yako. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Amina.

²⁶² Njoo, ndugu, vivyo hivyo, nenda moja kwa moja chini ya msalaba, ukiamini. Katika Jina la Yesu Kristo, tujalie. Hiyo ni kweli.

²⁶³ Njoo, dada yangu. Mwamini Mungu. Usiwe na shaka. Amini. Katika Jina la Yesu Kristo, naomba ombi lake lijibiwe. Amina.

²⁶⁴ Ombeni, ndugu. Kila mmoja aombe, kila mahali. Vema. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia dada yangu aponywe.

²⁶⁵ Njoo, dada. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Amina. Njoo, yeyote yule huyo anayeomba, mwanamume fulani huko nje, endelea kuomba.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Mwaminini Mungu.

Njoo, dada. Amini sasa, kwa moyo wako wote. Katika Jina la Yesu, na uponywe.

Njoo, ndugu yangu. Unaamini? Mtu mkubwa mno, mwenye nguvu, lakini hata hivyo, akiwa na tatizo la tumbo. Amini kwa moyo wako wote, na uende nyumbani, upone katika Jina la Bwana Yesu. Vema, bwana.

Unaamini, dada mdogo? Vema, njoo kwangu hapa. Katika Jina la Bwana Yesu naomba haja yake itimizwe.

Amini, ndugu yangu, kwa yote yaliyo ndani yako. Katika Jina la Yesu Kristo, haja yako na itimizwe. Usiwe na shaka; endelea, unaweza kuona . . . ? . . . Njoo.

Mungu akubariki. Asante bwana . . . ? . . . Ni sawa, sivyo?

Unaamini kwa moyo wako wote? Mungu akubariki, kijana mwanamume. Katika Jina la Yesu na uponywe.

Njoo, dada. Huu ndio mwisho wa kadi za maombi? Kwani kadi zote za maombi zimekwisha? U hali gani? Uniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Unaamini. Unaamini basi Yeye anaweza kuniambia yote kuhusu tatizo lako? Vema. Sasa, ninaamini ndio kwanza useme umetoka hospitalini sasa hivi. Moja ya shida zako, una nyonga iliyolemaa, tatizo kwenye nyonga yako. Lakini kwenda hospitalini kwako kulikuwa ni kwa ajili ya upasuaji wa kike; hapajapona bado. Hiyo ni kweli,

sivyo? Nalo jina lako ni Bibi Potts. Wewe nenda zako nyumbani ukapone sasa...?...

²⁶⁶ Unaamini kwa moyo wako wote? Kuwa na imani. Mtu huyo aliyeketi huko nyuma kabisa ndiye ninayeendelea kumwona. Yeye anaomba... Amevaa shati jeupe, limefunguliwa kwenye ukosi, akimwomba rafiki yake aliyeketi nyuma yake pale akiwa na tatizo la ubongo. Unaamini, bwana? Simama kwa miguu yako na kuukubali. Weka mikono yako juu ya rafiki yako hapo. Haya basi. Mungu akubariki. Nenda nyumbani ukawe mzima, mwanangu. Yesu Kristo anakuponya. Haleluya. Alikuwa akimwomba rafiki yake. Hilo ndilo linalolifanya. Yesu Kristo, Mwana wa Mungu hufanya mambo haya, anawaponya. Mnaamini hilo?

Huyu hapa mwanamke ameketi papa hapa amejifunga kitu kidogo cheupe kichwani, ameketi papo hapo karibu na msichana aliye na kitu kinachoonekana cha bluu nyweleni mwake. Huyu mwanamke anamwomba mume wake. Hiyo ni kweli. Huyu mume alikuwa na kansa, nawe unahofu inamrudia tena. Hiyo ni kweli, sivyo? Vema. Unaamini? Simama kwa miguu yako basi, likubali. Katika Jina la Yesu Kristo, naomba imwache.

²⁶⁷ Mwombee mtu fulani. Mwombee rafiki. Mwombee mtu fulani. Hapa, huko nyuma kabisa, ninamwona mwanamume ameketi nyuma ya mwanamke huyu hapa, huko nyuma kabisa, ameketi ndani, wa pili aliyeketi mle ndani, anamwomba mke wake. Amerukwa na akili. Unaamini, bwana? Vema, simama kwa miguu yako na uukubali uponyaji wako, na uamini kwa moyo wako wote. Nenda nyumbani ukamkute akipata nafuu. Mungu akubariki, ndugu yangu mpendwa. Amini kwa yote yaliyo ndani yako.

Mtu mwingine yeyote anaamini? Mwaminini Mungu. Hapa, maskini msichana mdogo aliinua mkono wake papa hapa. Ile pale Nuru inayoning'inia juu yake. Loo, yeye ni... Huyu hapa maskini nanii... Kuna wawili. Maskini huyo mama aliinua mkono wake. Maskini huyo mama aliyeketi karibu naye, inaonekana kana kwamba hiyo Nuru inaning'inia juu ya maskini mama huyo mwenye nguo inayoonekana ya samawati. Unamwomba mtu fulani: mpwa wako, ana tatizo la moyo, wasiwasi. Hiyo ni kweli, sivyo? Hayupo hapa. Yuko Los Angeles. Huyu ni dada yako, hiyo ndiyo sababu ni uhusiano wa karibu sana. Yeye anaomba pia, bali ni kwa ajili ya rafiki. Anaomba kwa ajili ya wongofu wa rafiki huyu. Rafiki huyu ni Mkatoliki, naye anamwomba. Hiyo ni kweli. Nyote wawili ni dada. Endapo hiyo ni kweli, simameni kwa miguu yenu. Mungu awabariki. Sikujui, sijawahi kukuona maishani mwangu. Kuna kitu fulani cha kigeni kukuhusu hata hivyo. Ama umekuwa mahali fulani, au—au unamjua mtu fulani kutoka mahali fulani ambapo nimekuwa. Ninaona mahali panapoonekana pa kigeni. Si—si hata... Ni Ujerumani. Hivi wewe ni Mjerumani? Hiyo ni kweli. Ndivyo

ulivyo. Hiyo ni kweli kabisa. Vema, imani yako imekupa haja yako. Nenda nyumbani. Utalikuta jinsi ulivyoamini. Haleluya.

²⁶⁸ Ninawapa changamoto, katika Jina la Yesu Kristo, kuamini Hilo kuwa ni kweli. Ninawapa changa...Jinsi...Kuna mwenye dhambi hapa angetaka kuja hapa na kusimama kabla hatujaendelea mbele zaidi na mstari wa maombi? Rafiki mwenye dhambi, wewe ambaye umerudi nyuma, ungetaka kumjua Bwana Yesu kama Mwokozi wako binafsi? Njoo hapa dakika moja tu wakati piano inapotuchezea wito mdogo mzuri wa madhabahuni. Njoo hapa. Roho Mtakatifu anajua wewe ni nani. Kama unamhitaji Kristo sasa hivi maishani mwako, waweza shuka uje kwenye wakati huu tu na kusimama hapa madhabahuni? Huu ungekuwa ndio wakati wa mwisho ambao kamwe nitapata kuomba pamoja nanyi siku zote za maisha yetu. Hii ndiyo nafasi yako. Mungu akubariki, jamaa mdogo.

Utakuja? Mtu mwingine? Mtu huyu anayekuja hapa. Mtu mwingine? Shuka moja kwa moja nyuma ya skrini hapo, na uje moja kwa moja madhabahuni sasa, wakati tukiingojea kwa dakika moja. Tutangojea. Njoo papa hapa, bwana, na usimame papa hapa.

Mtu mwingine angetaka kuja na kusimama karibu naye? Jitokezeni. Pandeni huku sasa na msimame hapa, ili tuweze kuwaombea. Nitafurahi. Nitafurahia sana kuomba pamoja nanyi. Njoni tu. Hivyo tu ndivyo tunavyowaomba kufanya.

Mungu akubariki, bwana, simama papa hapa. Kuna mwingine?

²⁶⁹ Kuna chemchemi iliyojaa Damu iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli, ambamo wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya mafuriko hayo hupoteza doa lao la hatia. Je, Mungu yuko katika ulimwengu Wake? Mungu katika Neno Lake? Mungu katika Mwanawe? Sasa, je, Mungu yuko ndani ya watu Wake? Vema, Mungu yuko papa hapa basi. Yeye anataka kuingia ndani yenu. Hivi hamtakuja?

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Iliyotolewa (...?..)

Wanapoteza madoa yao yote ya hatia.

Mtakuja sasa hivi, ninyi ambao mnamhitaji Kristo? Hatujali wewe ni wa kanisa lipi, ama ni lipi unalohudhuria, au ni lipi utakalohudhuria. Njoo. Hiyo ni kweli. Sogea moja kwa moja karibu na madhabahu sasa. Ninyi msio na Roho Mtakatifu, mnetaka kuja? Njoni moja kwa moja sasa wakati tukiimba. Njoni.

Na wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya
gharika hilo,
Hupoteza ninii yote...

Mungu akubariki, kipenzi. Nina mtoto Sarah nyumbani yapata umri wako. Unaona hilo, mama?

Wanapoteza madoa yao yote ya hatia,

Mungu akubariki, dada. Umeshawishika ya kwamba Kristo yuko ndani ya watu Wake? Njoo huku mbele sasa, sivyo? Jitokeze moja kwa moja. Njoo huku.

Na wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya gharika hilo,

Hupoteza madoa yao yote ya hatia.

Mwivi anayekufa alifurahia kuona

Chemchemi hiyo katika siku yake;

Kristo ametolewa kwako, rafiki. Utakuja na kumpokea?

. . . nijalie mimi, ingawa . . .

Mungu akubariki. Hilo ni zuri. Tembea moja kwa . . .

Nioshe na kuondolea mbali dhambi yangu yote.

Nioshe na kuondolea mbali dhambi yangu yote,

Nioshe na kuondolea mbali dhambi zangu zote;

Na hapo naomba mimi, ingawa ni mwovu kama yeye,

Nioshe na kuondolea mbali dhambi zangu zote.

²⁷⁰ Kwa hiyo nitakuwa na hakika ya kwamba hakuna mikono iliyojaa damu kwenye siku ya hukumu itakayokuwa ikiniashiria na kusema, “Ungeshikilia muda mrefu zaidi kidogo,” ninaomba na kumwalika kila mtu asiye na Kristo, asiye na tumaini, asiye na Roho Mtakatifu, katika Jina la Yesu Kristo, ninawaalika hapa kwenye madhabahu hii. Njoo ukampokee sasa. Lakini usipompokea, basi sitawajibika kwenye siku ya hukumu. Fanyeni hivyo sasa, wakati Kristo akiwa miongoni mwetu. Tunatambua hilo.

Mungu yuko katika ulimwengu Wake. Mnamwona huko nje. Mungu yuko katika Neno Lake. Mnamwona hapa. Mungu yuko katika Mwanawe. Mnamwona msalabani. Mungu yuko katika watu Wake. Mnamwona hapa akitenda kazi, akifanya kazi, Yuko hapa.

Sasa, hebu tuje wakati tukiimba mara nyingine moja, *Kuna Chemchemi Iliyojaa Damu*. Si mje?

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,

Hii hapa ile chemchemi, hapa msalabani. Si mje?

. . . mishipa ya Imanueli,

Na wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya mafuriko hayo,

Hupoteza madoa yao yote ya hatia. (Mungu akubariki.)

... madoa yao yote ya hatia,
Hupoteza madoa yao yote ya hatia;
Na wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya
mafuriko hayo,
Hupoteza madoa yao yote ya hatia.

²⁷¹ Endeeleni tu kuja. Hiyo ni sawa. Endeeleni kusonga. Tutaendelea kungojea. Tunao muda mwingi sana kuwangojea wagonjwa waje madhabahuni. Njoni moja kwa moja. Tu wenye furaha, tumefurahi, tunamshukuru Mungu kwamba mnakuja. Njoni huku moja kwa moja sasa Mbele za Roho Mtakatifu, Yeye aliyeenea kila mahali, mwenye nguvu zote, asiye na kikomo. Naomba mje Kwake sasa wakati neema Yake inabubujika vya kutosha kuwaokoa nyote, kuwapa kila kitu mnachohitaji. Yeye yuko hapa kuwapa Roho Mtakatifu, kuyaokoa maisha yenu, kuwaponya ugonjwa wowote, kuwafanyia chochote mtakacho. Bwana abariki.

²⁷² Sasa, wakati kusanyiko likiomba, kimoyomoyo, nitazungumza na wale waliopo hapa. Marafiki, kitu Fulani kiliwaambia mje kwenye madhabahu hii. Ilikuwa ni Yule yule anayejua moyo wenu, Yule yule anayenena hapa, Roho Mtakatifu, Mungu. Mungu ni Roho Mtakatifu katika watu Wake, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.

Sasa, Yeye amekuja kuwapatania kwa nafsi Yake. Heri ninyi. Heri macho yaliyofunguliwa kuuona Ufalme wa Mungu. Kumekuwako na maelfu mengi ya watu wenu mbele zenu, mamia na mamia ya babu zenu, waliotamani kuziona siku hizi. Watu wengi mashuhuri mbele yetu, watu wengi mashuhuri mbele yenu walitamani kuona wakati ambapo Roho Mtakatifu angeingia kanisani na kufanya yale mliyoyaona yakifanywa alasiri ya leo. Walikufa katika imani, wakiadini ya kwamba siku moja watoto wao watauona.

Sasa, mmeuona alasiri ya leo. Mmelisikia Neno. Mnajua ni kweli. Naye Mungu ameyafungua macho yenu; maombi yao.

²⁷³ Hawa hapa wasichana wadogo waliosimama hapa, mama amesimama, akiwashika wasichana wawili wadogo. Watoto wadogo wamekuja huku, wakilia. Nashangaa kama mtoto, watoto, wakati mwingine hawawahukumu watu wazima, kutoka kwenye maskini moyo wao mwororo. Hawajaupitisha kwenye kila namna ya masikitiko ya ulimwengu na kadhalika. Ni mwororo na mzuri. Ninawatazama wasichana hawa wawili waliomkumbatia huyu mama, kama tu walikuwa wakitajaraja jambo fulani kutukia. Hakika, Mungu huwazungumzia watoto Wake wadogo. Biblia ilisema hivyo. "Acheni watoto wadogo waje Kwangu. Msiwakataze."

Ninamwona maskini mama hapa amemshika mtoto wake mchanga, mtoto mchanga anayependeza, amemshika mikononi mwake. Amekuja hapa sasa apate kupatanishwa kwa Kristo. Sasa, heri wewe. “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu...”

Kijana mwanamume akimshika mke mdogo, nadhani, amesimama pale amemshika. Mke analia. Mume ameinamisha kichwa chake katika uchaji. Hivi mnajua hiyo ni kazi ya Roho Mtakatifu? Wengine, maskini msichana mwenye macho ya hudhurungi akiniangalia yapata umri wa miaka saba ama minane, macho madogo ya hudhurungi na nywele za hudhurungi, maskini uso wake wote umechangamka. Anatarajia kitu fulani. Huenda akawa ni Mhispania.

²⁷⁴ Ninamwona maskini msichana wa kupendeza, kwenye njia panda tu za maisha huku amekiinamisha kichwa chake kwa kicho, mikono yake imekunjwa. Ninawaona wengine, nywele zenye mvi, vichwa vyao vimeinamishwa. Huu ni wakati mtukufu.

Kumbukeni, marafiki, kamwe hatuji hapa juu ati kuja tu. Tumekuja kwa sababu Mungu alikuia. Ninyi ni kumbukumbu za mkutano huu alasiri ya leo. Kwa kweli, ninyi ni kumbukumbu za neema ya Yesu Kristo, ambapo Yeye amewaita mpate kupatanishwa na kuja kumpokea alasiri ya leo. Mungu awe nanyi.

“Heri wao (Mnaona?) wenye njaa na kiu ya haki. Watashibishwa.” Unapata hayo katika zile Heri. Yesu alisema hivyo.

Vijana wanaume wamesimama hapa, vijana wanaume tu, labda umri wa miaka kumi na minane, ishirini, labda wahubiri wa siku za usoni, ninajuaje? Labda kutoka hapo atatoka mmishenari atakayeuangazia ulimwengu. Labda kutoka kwenye hao vijana wanaume kutatokea karama ambazo zitavuta maelfu ya nafsi kwa Kristo, nanyi mlikuwako siku walipokuja madhabahuni. Ni wakati wa ajabu jinsi gani.

²⁷⁵ Na tuinamishe vichwa vyetu sasa, wakati nikiomba dua. “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu,” alisema Yesu, “asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Na wote wanijiao Mimi, sitawatupa nje kamwe. Njoni Kwangu ninyi nyote msumbukao na mliolemewa na mizigo mizito. Nitawapa raha.”

Bwana, hawa hapa. Wamekuja kwa sababu Wewe umewaita waje. Roho Mtakatifu moyoni mwao ametenda kazi na kuwaita, nao wamekuja. Hawa hapa wamesimama madhabahuni, wenye subira, wameviinamisha vichwa vyao, wakitaka kujazwa na Roho Wako wa wema Wa—Wako. Wajaze, Bwana. Yatakase maisha yao. Watume kwenye mashamba ya mavuno, watu hawa waliosimama hapa wakingojea. Huenda ikawa tu ni nyumbani. Huenda ikawa ni ng'ambo ya bahari. Huenda ikawa ni mahali fulani, bali kuna mavuno yaliyo tayari kuvunwa.

Bwana, ninaomba ya kwamba Wewe utazitakasa nafsi zao, na kuwajaza na Roho, mpaka watakuwa vyombo Vyako vilivyochaguliwa: labda maskini mke wa nyumbani kuwavuna majirani, labda mtoto mdogo amwambie msichana mdogo habari za Yesu shuleni, labda vijana wanaume waipeleke Injili Meksiko, nchi nyingine ya kigeni mahali fulani. Tujalie, Bwana. Mzee kumzungumzia rafiki yake kando ya barabara, labda mahali pengine, mtu wa kiwanda kwa bosi wake, ama kwa wale walio kiwandani. . . Wewe unajua, Bwana. Ninaomba kwamba Wewe utawajaza sasa hivi, kwa wema Wako na rehema.

Wamekuja; ninajua Wewe umewapokea, kwa sababu Wewe ulisema, “Yeye anijiaye Mimi, sitamptupa nje kamwe. Yeye atakayenikiri Mimi mbele ya watu, huyo nitamkiri mbele ya Baba Yangu, na Malaika watakatifu.” Kwa hiyo, wako hapa wamesimama hadharani kukiri: walikuwa makosani. Wanataka kuwa sawa. Wewe wapokee, Baba. Ninaomba ya kwamba utawabariki, na kuwafanya watoto Wako tangu sasa na kuendelea, kupitia Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁷⁶ Mungu awabariki, kila mmoja wenu. Mpokeeni Roho Mtakatifu. Sasa, ingieni moja kwa moja mle chumbani ambamo tunaweza kukutana nanyi huku nyuma, na kumwekea mikono kila mmoja wenu, kuomba. Papa hapa nyuma, rudini moja kwa moja nyuma. Kuna chumba kilichoandaliwa hapa nyuma, ambamo mtakuwa katika dakika chache pale nyuma kwa ajili ya ku—kujazwa kabisa. Piga magoti; mshukuru Mungu kwa kukuokoa. Mtawekewa mikono huko nyuma kwa ajili ya haja yako, na kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Mungu awabariki. Mbariki maskini mama huyu, wote wakienda huku wamewabeba watoto wao wachanga, naye baba akizipapasa nywele za mtoto wake mchanga, akijua ya kwamba yeye pia anajua kwamba siku moja anaweza kumwambia mtoto wake mdogo, tuliketi kwenye mkutano ule ambapo walimjia Bwana Yesu. (*Mahali Pa Raha Hivi Karibuni.*)

Kuna Nchi ambayo ni nzuri kuliko mchana,
Na kwa imani tunaweza kuiona kwa mbali.
Kwa maana Baba anasubiri njiani,
Kutuandalia makazi Kule.

Mahali pa raha hivi karibuni,
Loo, tutakutana kwenye Pwani hiyo nzuri.
Mahali pa raha hivi. . . 

59-1129 Na Tumwone Mungu
Santa Clara County Fairgrounds
San Jose, California Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org